# MATUMIZI YA MBINU INAYOTEGEMEA SHUGHULI ZA MWANAFUNZI KATIKA UFUNDISHAJI WA RIWAYA KWA SHULE ZA UPILI KATIKA KAUNTI YA MAKUENI, KENYA

**JULIENS MUMANGI KOKA**

**E55/CE/28028/2013**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA ELIMU, KITIVO CHA ELIMU, CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**OKTOBA 2021**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine chochote kwa mahitaji ya shahada ya uzamili.

…………………………………… …………………………….

JULIENS MUMANGI KOKA TAREHE

E55/CE/28028/2013

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

…………………………………………… ………………………….

DKT. HAMISI OMAR BABUSA TAREHE

IDARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA ELIMU

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

…………………………………………… ………………………….

DKT. FLORENCE ABUYEKA MIIMA TAREHE

IDARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA ELIMU

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

# TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu wapendwa mamangu Beth na babangu Koka kwa kujitolea mhanga kunilea, kunisomesha na kunitia motisha masomoni kila mara.

# SHUKRANI

Ukamilishaji wa kazi hii hautokani na juhudi zangu pekee mbali pia za watu mbalimbali. Ni kweli kuwa, ‘‘jifya moja haliinjiki chungu”. Nitakuwa mtovu wa nidhamu ikiwa nitawasahau wale waliojitolea kwa hali na mali kuifanikisha ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili.

Namshukuru Maulana kwa kunipa siha nzuri mwilini, hekima na uvumilivu wa kupambana na changamoto zote katika safari hii ngumu ya masomo. Nawashukuru pia walimu na wasimamizi wa kazi yangu Daktari Miima na Daktari Babusa kwa uelekezi wenu kipindi kizima cha utafiti wangu. Kwa kweli bila usaidizi wenu singefika hapa. Mwenyezi Mungu awalinde maishani. Wahadhiri wote idarani mlioshiriki kunielekeza ahsanteni.

Kwa mke wangu Patricia, binti zangu June na Praise shukrani za dhati ziwafikie. Mlivumilia na kujinyima mambo mengi wakati wa kipindi cha masomo yangu. Mungu awabariki. Rafiki wangu wa karibu Phyllis, ulinitia moyo kila wakati kuwa nitie bidii ili nikamilishe kisomo hiki. Ahsante kwa hayo.

Ndugu zangu na masahibu wangu; John, Gregory, Shadrack, Jenniffer na Phoebe, tulihimizana sana masomoni. Asanteni kwa usaidizi wenu, Rabana awajalie neema aushini. Wale wote ambao sijawataja nasema ahsanteni kwa kunishika mkono na kunitia moyo hadi nikafikia hatua hii ya mwisho.

## YALIYOMO

**UNGAMO……………………………………………………………….ii**

**TABARUKU…………………………………………………………...iii**

**SHUKRANI…………………………………………………………….iv**

**YALIYOMO……………………………………………………………….v**

**ORODHA YA MAJEDWALI………………………………..……….....ix**

**ORODHA YA MICHORO………………………………………………..x**

**FASILI YA VIFUPISHO…………………………………………………xi**

**IKISIRI…………………………………………………………………...xii**

**SURA YA KWANZA:UTANGULIZI NA USULI WA MADA YA UTAFITI………………………………..……..…1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................ 1

1.2 Usuli wa Utafiti ................................................................................ 1

1.3 Swala la Utafiti ................................................................................ 6

1.4 Lengo la Utafiti................................................................................ 6

1.5 Madhumuni ya Utafiti ..................................................................... 7

1.6 Maswali ya Utafiti ........................................................................... 7

1.7 Umuhimu wa Utafiti........................................................................ 7

1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti .............................................................. 9

1.8.1 Upeo wa Utafiti ............................................................................. 9

1.8.2 Mipaka ya Utafiti.......................................................................... 10

1.9 Makisio ya Utafiti............................................................................ 10

1.10 Nadharia ya Utafiti ........................................................................ 11

1.11 Mgofu Dhanifu wa Utafiti............................................................. 15

1.12 Ufafanuzi wa Istilahi ..................................................................... 17

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI………………………….. 18**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 18

2.2 Mbinu za Ufundishaji wa Fasihi ........ 18
2.2.1 Mbinu zinazomwegemea zaidi Mwanafunzi ........ 19
2.3 Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 21
2.3.1 Hatua Mbalimbali za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 24
2.3.2 Sifa za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 27
2.4 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 28
2.5 Ufundishaji wa Riwaya ........ 29
2.6 Ufaafu wa Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 30
2.7 Changamoto za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........ 32
2.8 Tafiti zilizoandikwa kuhusiana na Mada ........ 33
2.9 Pengo la Utafiti ........ 36
**SURA YA TATU:MUUNDO NA MBINU ZA KUKUSANYA DATA… 38**
3.1 Utangulizi ........ 38
3.2 Muundo wa Utafiti ........ 38
3.3 Vigeu vya Utafiti ........ 39
3.4 Eneo la Utafiti ........ 39
3.5 Watafitiwa Lengwa ........ 40
3.6 Sampuli na Mchakato wa kuteua Sampuli ........ 41
3.7 Mbinu na Vifaa vya Utafiti ........ 42
3.7.1 Hojaji kwa Walimu ........ 42
3.7.2 Mahojiano ........ 43
3.7.3 Mtihani wa Mwanzoni na Mwishoni mwa Utafiti ........ 43
3.7.4 Mwongozo wa Uchunzaji ........ 44
3.8 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti ........ 45
3.8.1 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti ........ 46

3.8.2 Utumainifu wa Vifaa vya Utafiti ..................................................... 47
3.9 Utaratibu wa kukusanya Data .................................................................. 48
3.10 Uchanganuzi wa Data .............................................................................. 49
3.11 Uwasilishaji wa Data ............................................................................... 50
3.12 Maadili katika Utafiti ............................................................................... 50
**SURA YA NNE:UWASILISHAJI WA DATA, UCHANGANUZI NA MAJADILIANO……………………………………52**
4.1 Utangulizi .................................................................................................. 52
4.2 Ujumla wa Data na Usuli wa Wahojiwa .................................................. 53
4.2.1 Kiwango cha Urejeshaji wa Vifaa vya Utafiti ................................. 53
4.2.2 Usuli wa Wahojiwa ......................................................................... 53
4.3 Mbinu zinazotumiwa na Walimu wa Fasihi kufundishia Riwaya ............ 58
4.4 Kiwango ambacho Walimu wa Fasihi hutumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ............................................................................ 60
4.5 Athari za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Utendaji wa Wanafunzi ........................................................................................... 61
4.5.1 Utendaji kwa Kutegemea Jinsia ............................................................ 63
4.6 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ............................................................................................. 65
4.7 Changamoto wanazokabiliana nazo Walimu wanapotumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi .................................................. 67
**SURA TA TANO:MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.71**
5.1 Utangulizi .................................................................................................. 71
5.2 Muhtasari wa Matokeo ............................................................................... 71
5.2.1 Mbinu zinazotumiwa na Walimu wa Fasihi kufundisha Riwaya ........... 71
5.2.2 Kiwango ambacho Walimu wa Fasihi hutumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ............................................................................ 72

5.2.3.1 Athari za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Utendaji wa Wanafunzi ................................................................ 73

5.2.3.2 Utendaji wa Wanafunzi kwa kutegemea Jinsia ........................ 74

5.2.4 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ........................................................................................ 74

5.2.5 Changamoto wanazokabiliana nazo Walimu wanapotumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ................................................. 75

5.3 Hitimisho ............................................................................................ 76

5.4 Mapendekezo ....................................................................................... 77

5.5 Mada zinazopendekezwa kwa Utafiti zaidi ............................................ 79

**MAREJELEO** ........................................................................................ 80

**VIAMBATISHO** ……………………………............................................. 85

KIAMBATISHO CHA 1: Hojaji Kwa Walimu…………………………… 85

KIAMBATISHO CHA 2: Mwongozo wa Uchunzaji Darasani…………..…91

KIAMBATISHO CHA 3: Mahojiano na Walimu wa Fasihi, Kidato cha Tatu……………………………………….........92

KIAMBATISHO CHA 4: Mtihani Tangulizi (Pre-Test)…………….…...93

KIAMBATISHO CHA 5: Mtihani wa Mwishoni (Post – test)…………….94

KIAMBATISHO CHA 6: Barua ya Ukubalifu wa Pendekezo la Utafiti (Chuo Kikuu cha Kenyatta)………………………95

KIAMBATISHO CHA 7: Barua ya Idhini ya Utafiti (Chuo Kikuu Cha Kenyatta)……………………………………......96

KIAMBATISHO CHA 8: Kibali cha Utafiti (NACOSTI)…………..…....97

KIAMBATISHO CHA 9: Barua ya Idhini (NACOSTI)………………….....98

KIAMBATISHO CHA 10: Barua ya Idhini (Mkuu wa Kaunti, Makueni)….99

KIAMBATISHO CHA 11: Barua ya Idhini (Mkurugenzi wa Elimu, Makueni)...........................................................100

KIAMBATISHO CHA 12: Ramani ya Kaunti -Ndogo ya Mukaa…………101

## ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI 1. 1**: Matokeo ya Mtihani wa Fasihi wa KCSE nchini, kati ya Mwaka....................................................................... 3

**JEDWALI 1. 2:** Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa KCSE katika Kaunti-ndogo tisa, Kaunti ya Makueni kati ya Mwaka 2014 - 2017……………………………………...…………..…..4

**JEDWALI 3. 1:** Uteuzi wa Sampuli ............................................................ 42

**JEDWALI 4. 1:** Kiwango Cha Urejeshaji Wa Vifaa Vya Utafiti .................. 53

**JEDWALI 4. 2:** Aina ya Shule Zilizoshirikishwa kwenye Utafiti huu.......... 54

**JEDWALI 4. 3:** Kiwango cha Matumizi ya Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Juma. ..................................................... 60

**JEDWALI 4. 4:** Matokeo Ya Mtihani Wa Mwishoni Mwa Utafiti ............... 62

**JEDWALI 4. 5**: Utendaji kwa kutegemea Jinsia .......................................... 65

**JEDWALI 4. 6:**Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi ................................................... 66

**JEDWALI 4. 7:** Changamoto za Walimu katika Matumizi ya Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi. ............................ 68

## ORODHA YA MICHORO

**MCHORO 1. 1:** Mgofu Dhanifu wa Utafiti unaonyesha Vigeu huru, Vigeu ingilizi na Vigeu tegemezi. .................................................. 16

**MCHORO 4. 1:** Jinsia ya Walimu ................................................................ 55

**MCHORO 4. 2:** Kiwango cha elimu cha walimu wa fasihi .......................... 56

**MCHORO 4. 3:**Tajiriba ya Ufundishaji wa Fasihi kwa Walimu.................. 57

**MCHORO 4. 4:** Matumizi ya mbinu mbalimbali zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wa riwaya ................................................ 58

**MCHORO 4. 5:** Jinsia ya Wanafunzi walioshiriki katika Mtihani. ............... 64

**MCHORO 4. 6:** Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi. ...................................................................... 66

## FASILI YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **DIQASO** | : | Directorate of Quality Assurance and Standards Officer. |
| **KNEC** | : | Kenya National Examination Council. |
| **KCSE** | : | Kenya Certificate of Secondary Education. |
| **UNESCO** | : | United Nations Educational, Science and Cultural Organisation. |
| **TATAKI** | : | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. |
| **NACOSTI** | : | National Commission for Science, Technology and Innovation. |
| **SPSS** | : | Stastical Package for Social Sciences. |

# IKISIRI

Mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji huchangia pakubwa uelewa wa mwanafunzi na kile kinachofundishwa. Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza namna mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inavyotumiwa katika kufundishia riwaya ya Kiswahili. Mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji darasani huathiri pakubwa kiwango cha uelewa wa wanafunzi wa kile kinachofundishwa. Utafiti huu ulidhamiria kutimiza madhumuni yafuatayo: kubainisha mbinu zinazotumiwa kufundishia riwaya, kuchunguza ni kwa kiwango kipi walimu wa fasihi wanatumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, kuchunguza athari za mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kwa utendaji wa wanafunzi, kubainisha mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi na kutambua changamoto za walimu wanapotumia mbinu husika. Utafiti huu ulifanyika katika kaunti ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni. Utafiti uliongozwa na nadharia ya ubunaji. Uchanganuzi wa data ulifuata muundo wa kimaelezo. Mtafiti alitumia uteuzi makusudi kuteua shule katika viwango vya kitaifa, kaunti na kaunti ndogo. Idadi ya watafitiwa katika utafiti huu ilihusisha sampuli lengwa na sampuli mahususi. Sampuli lengwa ilikuwa shule 43, walimu 60 na wanafunzi 2850. Uteuzi makusudi ulitumika tena kuteua madarasa ya wanafunzi na walimu wao. Nayo idadi mahususi ilikuwa shule 6, walimu 12 na wanafunzi 540. Data ilikusanywa kutumia: hojaji, mahojiano uchunzaji darasani na mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti. Data ilichanganuliwa kwa muundo wa kimaelezo, kithamani na kiidadi. Data hiyo iliwasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali na grafu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa walimu wengi hutumia mbinu za kawaida na ambazo walizizoea mno katika ufundishaji wa riwaya kama vile mbinu ya mhadhara na ya masaili. Aidha mbinu zinazowashirikisha zaidi wanafunzi ziliepukwa sana na walimu. Mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi haikutumiwa sana na walimu. Ilibainika wazi kuwa wanafunzi wanapofundishwa kwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huelewa vyema kuliko vile wanavyoelewa wakifundishwa kwa mbinu za kawaida. Walimu wengi walikuwa na mtazamo hasi kuhusiana na mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Pia walimu walikabiliwa na changamoto kadha wakati wa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wao ikiwepo changamoto ya ukosefu wa muda wa kutosha na kazi nyingi kwa walimu wanapotekeleza mbinu hiyo. Utafiti huu utakuwa wa umuhimu mkubwa kwa makundi mbalimbali ya watu katika eneo la utafiti yakiwemo yafuatayo: walimu wa fasihi katika shule za upili, maafisa wa kukadiria ubora wa viwango vya elimu, wanafunzi wa somo la fasihi, taasisi ya kukuza mtaala ya Kenya na mwisho kabisa kwa watafiti wengine ambao wangetaka kutafiti kuhusu ufundishaji wa riwaya. Kwa ujumla utafiti huu utaboresha ufundishaji wa riwaya katika shule za upili. Utafiti huu ulipendekeza walimu wafanyiwe mafunzo zaidi ili waweze kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wao wa riwaya na kukabiliana na changamoto zake. Mapendekezo zaidi yalifanywa ili kuweza kuimarisha ufundishaji wa riwaya.

# ABSTRACT

Teaching strategies used by teachers determine the degree of understanding of the content by the learners. Classroom instruction methods used affect to a great extend the understanding of the content by the learners. The purpose of this study was to find out how teachers use task-based method in teaching the Kiswahili novel. The objectives of this study were: - to find out the methods used in teaching of the Kiswahili novel, to investigate the extent to which literature teachers use task-based method of teaching, to find out the effects of task-based method of teaching on the understanding of the content by the learners, to identify teachers views regarding the task-based method of teaching and finally explore the challenges faced by teachers in the use of task-based method of teaching. The research was carried out in Mukaa sub-county, Makueni county. Constructivism theory was used. The researcher used Descriptive research design. The target population included 43 schools, 60 teachers and 2580 students. Purposive sampling was used to categorize the schools into three groups; National, Extra-County and County schools, then two schools from each category were sampled randomly. 12 teachers and 540 students were sampled purposively. Data was collected using; questionnaires, interviews, observation and pre-test and post-test. Quantitative data collected was analyzed using descriptive statistical techniques which included percentages and the mean while qualitative data was analyzed thematically. The collected data was then presented by use of narrations, tables and graphs. Findings of this study show that majority of teachers embloyed the commonly used methods of teaching such as question and answer and lecture method in teaching of the Kiswahili novel. In addition to this, the study showed that teachers avoided the use of learner-centered methods. Task based method of teaching was rarely used by majority of teachers. From the results of the study, it was clear that students understand the Kiswahili novel better while taught by use of task-based method as compared to the commonly used general methods. Furthermore, majority of the teachers had a negative attitude towards task-based method of teaching. Teachers were faced by several challenges while using task-based method such as lack of enough time to cover the syllabus and the high volumes of content to be taught. This research is of great importance to; literature teachers in secondary schools, quality assurance and standard officers, literature students, curriculum developers and lastly to other researchers interested in this area of study. In general, the research will go a long way in improving the teaching of Kiswahili novel in secondary schools in Kenya. This study recommended intense training for the teachers to perfect the use of task-based method of teaching and also to enable them overcome all the challenges associated with task-based method of teaching. More recommendations were also suggested aimed at improving the teaching of the Kiswahili novel.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI NA USULI WA MADA YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mtafiti alishughulikia usuli wa utafiti, swala la utafiti, lengo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na makisio ya utafiti. Aidha nadharia ya utafiti, mgofu dhanifu wa utafiti pamoja na ufafanuzi wa istilahi zilishughulikiwa pia.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Lugha ya Kiswahili ni lugha muhimu sana ulimwenguni. Lugha hii ilianza katika Afrika Mashariki na baadaye kuzagaa katika bara zima la Afrika. Hivi sasa lugha hii inatambulikana ulimwenguni kote. Kulingana na Musau na Chacha (2010), Kiswahili kimeenea si katika bara la Afrika tu lakini kote ulimwenguni. Hivyo basi, lugha hii kwa sasa ni lugha ya kimataifa. Ni kutokana na hali hii ambapo lugha ya Kiswahili inafundishwa na kutahiniwa katika taasisi mbalimbali za elimu ulimwenguni. Kulingana na katiba ya Kenya (2010), Kiswahili ni lugha rasmi na pia lugha ya taifa. Serikali ya Kenya ilitambua dhima ya Kiswahili katika maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, Kiswahili ni chombo muhimu cha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Inasemekana kuwa asilimia themanini ya watu nchini Kenya hutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku. Jambo hili limetambuliwa na shirika la kimataifa la UNESCO (Momanyi, 2007). Nchini Kenya lugha hii inafundishwa na kutahiniwa katika shule zote za msingi na za upili na katika baadhi ya vyuo vikuu.

Somo la Kiswahili kama linavyofundishwa katika shule za upili nchini Kenya limegawika katika insha, lugha na fasihi. Katika fasihi kuna fasihi andishi na fasihi simulizi. Miongoni mwa tanzu za fasihi andishi kuna utanzu wa riwaya.

Wamitila (2003), anaelezea maana ya riwaya kama kazi andishi ya fasihi ambayo kwa kawaida ni ndefu kuliko hadithi fupi. Urefu wa riwaya maana yake ni kwamba msuko simulizi umejengeka vizuri, kuna wahusika wengi, unaenea muda mrefu, mada zake ni nzito na pana kiasi. Licha ya somo la fasihi kuwa limefundishwa kwa muda mrefu, ufundishaji wake kwa dhati umebaki nyuma na ni finyu kama wanavyotambua wasomi Njogu na Chimerah (2008).

Somo la fasihi likiwa sehemu ya Kiswahili lina malengo yake ya kufundishwa. Mojawapo wa malengo hayo ni kuwawezesha wanafunzi kuupita mtihani wa Kiswahili kwa ujumla. Wanafunzi wanapopata alama nzuri katika mtihani huwa ni ishara ya kuelewa kwa undani kile kilichofundishwa.

Kulingana na Moshi (2006), ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili Marekani na Uropa ungali unakumbwa na changamoto. Mbinu zinazotumiwa na walimu kufundishia fasihi katika maeneo hayo hazijaimarika kabisa. Hill (2018) anasema kwamba uelewa wa fasihi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi katika mataifa ya ughaibuni ni wa kiwango cha chini mno. Wanafunzi wengi kutoka katika mataifa hayo huonyesha matokeo mabaya katika mitihani ya fasihi ya Kiswahili. Nchini Tanzania, uelewa wa fasihi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili ni wa kiwango cha juu (Hill, 2017). Kulingana na Bakize, Ngugi na Lyimo (2018), wanafunzi wengi nchini humo wanafanya vyema katika mitihani ya fasihi, jambo linaloashiria kuelewa kwao somo la fasihi.

Nchini Kenya, katika miaka ya hivi karibuni matokeo ya Kiswahili katika mtihani wa kidato cha nne wa kitaifa (KCSE) yamekuwa yakididimia katika nchi nzima (KNEC, 2017). Mtihani wa Kiswahili unajumlisha karatasi tatu; insha, lugha na fasihi. Baraza hilo la mitihani linaendelea kuelezea zaidi kuwa matokeo ya karatasi ya fasihi yanashuka kwa kiwango cha juu mno katika miaka ya hivi karibuni (KNEC,2017). Karatasi ya fasihi huchangia asilimia arobaini ya mtihani wa Kiswahili kwa ujumla. Hivyo basi, matokeo mabaya katika mtihani wa fasihi yanaathiri pakubwa matokeo ya karatasi nzima ya Kiswahili. Alama ya wastani ya mtihani wa Kiswahili kwa ujumla ilishuka kutoka 77.97/200 mwaka wa 2016 hadi 69.43/200 mwaka wa 2017 (KNEC,2017). Jedwali 1.1 linaonyesha matokeo ya mtihani wa fasihi katika kipindi cha miaka minne.

**Jedwali 1. 1: Matokeo ya Mtihani wa Fasihi wa KCSE nchini, kati ya Mwaka 2014 – 2017**

| MWAKA | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA $^{x}/_{80}$** | **42.93** | **38.80** | **25.67** | **25.15** |

**Asilia:** Ripoti ya KNEC (2017).

Katika kaunti-ndogo ya Mukaa, Kaunti ya Makueni, matokeo ya mtihani wa fasihi wa kitaifa yako chini ya alama ya wastani ya nchi nzima kati ya mwaka wa 2014-2017. Aidha eneo hili linaonekana kuwa na viwango vya fasihi vilivyo chini likilinganishwa na maeneo jirani. Yafuatayo ni matokeo ya mtihani wa fasihi ya Kiswahili katika kaunti-ndogo tisa, katika kaunti ya Makueni.

**Jedwali 1. 2:Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa KCSE katika Kaunti-ndogo tisa, Kaunti ya Makueni kati ya Mwaka 2014 - 2017**

| KAUNTI NDOGO/ ALAMA MWAKA (x/80) | MUKAA | KILUNGU | MAKINDU | NZAUI | KIBWEZI | MBOONI EAST | MBOONI WEST | MAKUENI | KATHONZWENI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2014** | **40.70** | **38.93** | **31.00** | **30.80** | **30.30** | **29.02** | **28.70** | **38.93** | **36.01** |
| **2015** | **32.20** | **41.80** | **32.30** | **32.90** | **32.80** | **32.90** | **29.20** | **40.91** | **38.20** |
| **2016** | **24.60** | **32.30** | **27.01** | **32.40** | **30.30** | **31.20** | **31.60** | **39.90** | **37.70** |
| **2017** | **22.40** | **33.50** | **28.20** | **30.50** | **32.60** | **33.80** | **31.90** | **37.90** | **37.90** |

**Asilia:** Afisi za elimu, kaunti ya Makueni.

Ahmad na Aziz (2009) wanasema kuwa wanafunzi wengi hawaelewi somo la Fasihi ya Kiswahili. Wanaendelea kusema kuwa hali hii inaweza kuwa imesababishwa na mbinu zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wao.

Kwa mujibu wa Calvert na Sheen (2015), ufundishaji wa fasihi unafaa kumshirikisha mwanafunzi zaidi katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Katika ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili kwa mfano, mwanafunzi anafaa kuhusishwa katika kusoma hadithi nzima kivyake bila kuwepo kwa mwalimu na hatimaye kutoa uchambuzi wake wa riwaya hiyo. Wanaelezea zaidi kuwa matumizi ya mbinu ya mhadhara na ya masaili katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili huwafanya wanafunzi kuwa wapokezi tu wa fasihi wakiwa katika hali tulivu. Mbinu

ya mhadhara inapotumiwa katika ufundishaji wa riwaya, mwalimu huwasomea wanafunzi hadithi huku wakisikiliza na hatimaye mwalimu huwachambulia wanafunzi hadithi hiyo huku wakinakili yale wanayoambiwa na mwalimu. Mara kwa mara wanafunzi hao wanaweza kuuliza maswali kuhusu mambo yasioeleweka kulingana na mhadhara huo.

Kulingana na Ahmad na Aziz (2009), ili wanafunzi wa fasihi waipende na kuielewa fasihi yenyewe vilivyo wanafaa kushirikishwa kikamilifu katika vipindi vya fasihi huku walimu wakiwa waelekezi tu. Zheng na Borg (2014) wanasema kwamba licha ya kuwa mengi yameandikwa kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji, utafiti kuhusu jinsi waalimu wanavyotumia mbinu yenyewe haujafanywa kikamilifu. Pulido, Catalina na Gonzalez (2016), wanasema kuwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumiwa katika ufundishaji, mwanafunzi huimarisha umilisi wake wa lugha ya mazungumzo na hali hii huchangia uelewa wake wa vitabu vya hadithi kwa kuwa anavisoma kwa ufasaha. Kulingana na Twoli, Maundu, Muindi, Kiio na Kithinji (2007), mbinu anazotumia mwalimu katika ufundishaji wake zinaweza kuathiri pakubwa uelewa wa wanafunzi wa kile wanachofundishwa.

Ni wazi kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya kile kinachofundishwa, jinsi kinavyofundishwa na uelewa wa wanafunzi kuhusu somo lenyewe. Kulingana na Twoli na Wenzake (2007), matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huwezesha mwanafunzi kuelewa kwa undani kile kinachofundishwa. Kutokana na madai haya, utafiti huu ulinuia kuchunguza namna mbinu hii inavyotumiwa na walimu katika kufundisha riwaya ya Kiswahili. Pia mtafiti aliweza kubaini uelewa wa wanafunzi wa riwaya wanapofundishwa kwa kutumia mbinu hii

na kulinganisha na uelewa wa wanafunzi hao hao wanapofundishwa kwa kutumia mbinu zingine.

### 1.3 Swala la Utafiti

Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi humshirikisha mwanafunzi kikamilifu katika shughuli nzima ya ujifunzaji na ufundishaji. Mwanafunzi anaposhirikishwa kikamilifu katika kipindi kuna uwezekano mkubwa wa kuelewa vyema kile kinachofundishwa (Twoli na Wenzake, 2007). Kwa mujibu wa Richards na Rodgers (2014), mwanafunzi anapofundishwa fasihi kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli anaweza kutakiwa kufanya mambo kadha peke yake kama vile kusoma riwaya, kuelezea sifa za wahusika, kujadili maudhui husika na fani miongoni mwa mengine. Ufundishaji wa somo la Kiswahili hasa fasihi unaendelea kukumbwa na changamoto si haba hapa nchini. Ripoti za KNEC za mitihani ya KCSE kuanzia mwaka wa 2014 hadi 2017 zinaonyesha kuwa matokeo ya somo la fasihi sio mazuri kote nchini. Katika eneo la kaunti ndogo ya Mukaa, matokeo hayo yako chini yakilinganishwa na matokeo ya kaunti-ndogo zingine katika kaunti ya Makueni. Kwa hivyo, utafiti huu ulinuia kuchunguza namna mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inavyotumiwa kufundishia fasihi. Aidha mtafiti alichunguza utendaji wa wanafunzi wa fasihi wanapofundishwa riwaya kwa mbinu hii na kulinganisha na mbinu zingine kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili.

### 1.4 Lengo la Utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza namna mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inavyotumiwa kufundishia riwaya ya Kiswahili katika kaunti-ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni.

## 1.5 Madhumuni ya Utafiti

i) Kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa fasihi kufundishia riwaya.

ii) Kuchunguza ni kwa kiwango kipi walimu wa fasihi wanatumia mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi katika kufundishia riwaya.

iii) Kuchunguza athari za mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi inapotumiwa kufundishia riwaya kwa utendaji wa wanafunzi.

iv) Kubainisha mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

v) Kuchunguza ikiwa kuna changamoto wanazokabiliana nazo walimu wanapotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

## 1.6 Maswali ya Utafiti

1) Ni mbinu zipi zinazotumiwa na walimu kufundishia riwaya?

2) Walimu huitumia vipi mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia riwaya?

3) Mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi ina athari gani kwa utendaji wa wanafunzi?

4) Walimu wana mitazamo gani kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi?

5) Ni changamoto zipi ambazo walimu hukumbana nazo wanapotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia riwaya?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Shughuli nzima ya ufundishaji wa riwaya katika shule za upili nchini Kenya inaweza ikakumbwa na changamoto kadha. Iwapo changamoto hizi hazikabiliwi na kudhibitiwa mapema zinaweza kuwa kikwazo kikubwa katika ufundishaji wa fasihi

miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini. Changamoto zikitokea katika ufundishaji ina maana kuwa malengo ya ufundishaji wa fasihi yenyewe hayataafikiwa. Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa kwa washikadau kadha katika sekta ya elimu nchini kama ifuatavyo:

Walimu wa fasihi katika shule za upili katika eneo la utafiti na kote nchini watafaidika pakubwa na utafiti huu kwa kuimarisha mbinu zao za ufundishaji wa riwaya. Walimu hao wataweza kutambua changamoto zote wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa riwaya ili kuweza kukabiliana nazo kwa njia mwafaka. Aidha, walimu wenyewe watatambua jinsi wanavyoweza kumshirikisha mwanafunzi vyema zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi katika shule za upili. Haya yote yatachangia pakubwa katika kuimarisha uelewa wa fasihi kwa wanafunzi wa shule za upili nchini.

Maafisa wa kukadiria ubora wa viwango vya elimu (DIQASO) katika kaunti ndogo ya Mukaa na kote nchini kwa ujumla watafaidika na utafiti huu barabara. Matokeo ya utafiti huu yataweza kuwasaidia pia maafisa hawa wa ubora wa viwango vya elimu ambao wataweza kuandaa warsha za walimu wa fasihi ili kuimarisha mbinu zao za ufundishaji. Jambo hili litawezekana tu baada ya maafisa wenyewe kutambua kuliko na mianya ya kuzibwa katika mchakato mzima wa ufundishaji wa fasihi katika shule za upili. Kwa kuandaa warsha za ufundishaji wa fasihi, watakuwa wanapiga hatua katika kazi yao ya kukadiria ubora wa viwango vya elimu na kuwarahisisishia walimu kazi yao kwa kuwaongezea maarifa zaidi ya ufundishaji.

Wanafunzi wa somo la fasihi katika shule za upili nao pia hawataachwa nyuma na utafiti huu. Wanafunzi hao wataweza kufaidika kutokana na shughuli za kuwashirikisha katika somo la riwaya zitakazopendekezwa na mtafiti. Aidha

shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi katika shule za upili inatarajiwa kuimarika kwa ujumla. Mbinu za kufundishia riwaya zikiboreshwa kulingana na mapendekezo ya mtafiti, mwanafunzi ataelewa somo lenyewe barabara.

Taasisi ya kukuza mitaala nchini Kenya (KICD) nayo pia itafaidika na utafiti huu. Taasisi hiyo inatarajiwa kufaidi kutokana na utafiti huu katika harakati zake za kuboresha silabasi ya fasihi katika shule za sekondari nchini. Silabasi yenyewe itaweza kuzingatia vipengele muhimu vya fasihi kulingana na utafiti wenyewe. Katika silabasi ya fasihi, malengo ya kufundishia somo la fasihi yataweza kuimarishwa kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wenyewe. Taasisi hii kupitia kwa wizara ya elimu itaweza kuwasaidia walimu fasihi ya Kiswahili hasa utanzu wa riwaya ili kuafikia malengo haya ya ufundishaji wa kipengele hiki cha fasihi miongoni mwa wanafunzi.

Mwisho kabisa, utafiti huu utawafaidi watafiti wengine watakaotafiti kuhusu ufundishaji wa riwaya na fasihi kwa ujumla. Watafiti hawa wataweza kuutumia kama msingi wa tafiti zaidi au wakarejelea matokeo yenyewe katika tafiti zao za baadaye. Aidha watafaidika kwa kuzingatia sehemu zitakazopendekezwa na mtafiti ili kufanyiwa utafiti zaidi.

## 1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti

### 1.8.1 Upeo wa Utafiti

Ingawa ufundishaji wa riwaya ya Kiswahili unaweza kufanywa kwa kutumia njia mbalimbali, utafiti huu ulijihusisha hasa mno na mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Utafiti huu ulilenga kutambua jinsi walimu wa Kiswahili katika kaunti-ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni nchini Kenya wanavyotumia mbinu

husika katika kufundisha riwaya ya Kiswahili. Aidha maoni ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na changamoto ambazo huenda wanakabiliana nazo wanapotumia mbinu hiyo ziliangaziwa pia. Vilevile ufundishaji wa Riwaya kwa kutumia mbinu hii ulilinganishwa na ufundishaji wa Riwaya iyo hiyo kwa kutumia mbinu za kawaida za ufundishaji na hatimaye mapendekezo yalitolewa kuhusu mbinu mwafaka zaidi inayopasa kutumiwa katika ufundishaji wa Riwaya. Sampuli ya utafiti iliteuliwa kutoka kwa walimu wa somo la Kiswahili katika eneo la utafiti pamoja na wanafunzi wa kidato cha tatu. Vifaa vya kukusanya data vilivyotumiwa katika utafiti huu ni pamoja na; hojaji, mahojiano, mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti na uchunzaji darasani. Inaaminika kwamba kwa kutumia vifaa hivi, mtafiti aliweza kupata data inayoweza kutumainiwa.

### 1.8.2 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihusisha tu shule za upili katika kaunti-ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni nchini Kenya. Ni katika shule hizi za upili ambako somo la fasihi hufundishwa. Wanafunzi wa kidato cha tatu pamoja na walimu wao ndio waliohusishwa ili kupata data inayostahili. Utafiti huu ulijikita tu katika malengo yake na vifaa vya kukusanya data vilivyochaguliwa.

## 1.9 Makisio ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na makisio yafuatayo:

i. Mbinu inayotumiwa katika ufundishaji huathiri shughuli nzima ya uelewa wa wanafunzi wa kile kinachofundishwa.

ii. Walimu wote wa fasihi katika shule husika hufundisha riwaya kama sehemu ya fasihi andishi katika kidato cha tatu.

## 1.10 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ndicho kioo cha kumulikia kila jambo au tendo limhusulo mwanadamu na jinsi anavyoishi ulimwenguni (Njogu na Chimera 2008). Nadharia hutuwezesha kuelewa falsafa ya kila binadamu. Bila nadharia, safari ya mwanadamu ulimwenguni inaweza kukumbwa na changamoto chungu nzima. Ni kutokana na sababu hii ambapo watu kadhaa kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni walibuni nadharia ili ziweze kuwaongoza maishani.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubunaji (1990). Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ina mihimili inayoweza kumsaidia na kumuongoza mtafiti katika utafiti wake. Kulingana na John (2018), nadharia hii iliasisiwa na Bruner (1990). Waasisi wengine wa nadharia hii ni pamoja na John Dewey (1998), Vygotsky (1978) na Jean Piaget (1972). Waasisi wa nadharia hii wanaamini kwamba zoezi la ufundishaji na ujifunzaji hukamilika vyema pale ambapo wanafunzi wenyewe wanashirikishwa kikamilifu katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji (Henson,2015). Mihimili ya nadharia hii ni pamoja na ifuatayo:

Uwezo wa binadamu wa kujua mambo yaliyo katika mazingira yake huwa nao kuanzia tumboni mwa mamake. Hivyo basi, binadamu anahitaji tu kushirikishwa kimazingira ili aweze kuukuza uwezo huo na kujua mambo mengi iwezekanavyo. Katika ufundishaji wa riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, mwanafunzi anafaa kuisoma riwaya akiwa peke yake naye mwalimu awe mwangalizi tu. Kwa kufanya hivyo, mwanafunzi ataweza kugundua mengi kuhusu riwaya yenyewe.

Mtu anajifunza tangu kuzaliwa hadi kuaga dunia. Kwa mujibu wa nadharia hii, hakuna wakati wowote katika maisha ya binadamu ambapo shughuli za kujifunza

mambo mapya hufikia kikomo. Kulingana na Amineh na Asl (2015), mwanafunzi wa fasihi anafaa kushirikishwa katika shughuli zinazomwezesha kujifunza fasihi yenyewe wakati wote maishani mwake. Mwanafunzi anafaa kushirikishwa na mwalimu kusoma riwaya nzima na kuchambua vipengele mbalimbali vya riwaya husika ili kuielewa zaidi.

Mwalimu na mwanafunzi ni watu wa kujifunza daima. Waasisi wa nadharia hii wanaamini kuwa mwalimu na mwanafunzi wote hujifunza bila kukoma kulingana na vile wanavyoingiliana na mazingira yao na kushirikishwa katika shughuli nyingi za kujifunza iwezekanavyo. Kwa hivyo, kulingana na kauli hii mwalimu na mwanafunzi wote wanaposhirikishwa katika shughuli za ujifunzaji na ufundishaji wa fasihi, wote wataendelea kusoma daima.

Mwanafunzi anapaswa kufundishwa mambo ambayo yeye mwenyewe anajua na kuelewa umuhimu wake maishani mwake (Bhattacharjee, 2015). Mwanafunzi anapaswa kuelezwa umuhimu wa fasihi ambayo anasoma ili iwe rahisi kwake kushiriki kikamilifu katika uchambuzi wa fasihi hiyo. Ufundishaji kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi humpa mwanafunzi nafasi ya kulinganisha maudhui yanayozungumziwa katika riwaya na matukio mbalimbali katika ulimwengu halisi.

Mwanafunzi anajifunza barabara zaidi kwa njia ya kuuliza maswali mara kwa mara na kutoa maoni yake. Waasisi wa nadharia hii wanaamini kwamba mwanafunzi anapouliza maswali na hatimaye kupewa nafasi ya kuweza kutoa maoni yake kuhusu suala husika huweza kujenga uaminifu ndani yake. Uaminifu huu humwezesha mwanafunzi kuelewa kwa urahisi na kile kinachofundishwa. Kulingana na Chang (2010), mwanafunzi anapotoa maoni yake kuhusu

kinachofundishwa hufanya hivyo kwa mtazamo mpana unaomwezesha kukihifadhi katika akili yake. Mbinu inayotafitiwa inampa mwanafunzi uhuru wa kutoa maoni wakati wa kipindi na pia kushiriki kikamilifu wakati wa kipindi chenyewe.

Aidha mhimili mwingine wa nadharia hii ni kwamba, jukumu la mwalimu katika kufundisha ni kujengea mwanafunzi msingi kutokana na busara zake. Wanaoshikilia nadharia hii wanaelezea kuwa mwalimu anafaa tu kumjengea mwanafunzi msingi katika ufundishaji. Kulingana na waasisi wa nadharia hii, msingi huu unapojengwa mwanafunzi anatakiwa kujifunza zaidi kwa kujivumbulia mambo huku akishirikishwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anapofundisha riwaya anafaa kuwaelekeza tu wanafunzi kuhusu yale wanayotarajiwa kuelewa kuhusu riwaya husika na kuwaacha huru kujisomea wenyewe. Pia mwalimu anaweza kuwaeleza wanafunzi msingi wa riwaya yenyewe kupitia kwa mambo kama vile historia na falsafa ya mwandishi.

Mtu hujifunza kwa ugunduzi na uvumbuzi. Mambo haya ya ugunduzi na uvumbuzi yanajengewa mazingira sababishi pale ambapo mwanafunzi anashirikishwa katika shughuli za kufundishia kikamilifu. Chang (2010), anasema kuwa wanafunzi wanaposhirikishwa katika ufundishaji na ujifunzaji wana uwezo wa kuvumbua mambo ambayo kamwe hayakuwa katika upeo wa fikira za mwalimu.

Mwalimu anafaa tu kuwaelekeza wanafunzi na kuwapa nafasi ya kujifunza na kujenga ubunifu (Amineh na Asl, 2015). Suala hili la kuwaelekeza wanafunzi ni mojawapo wa mambo muhimu yanayofanywa na mwalimu pale ambapo anafundisha kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Waasisi wa nadharia hii wanaamini kwamba pale ambapo mwanafunzi anaelekezwa tu na

kuachiliwa na mwalimu, basi hiyo huwa nafasi murua ya mwanafunzi husika kuonyesha ubunifu wake bila kuogopa chochote.

Mwanafunzi anapaswa kupewa uhuru wa kuteua fasihi anayotaka kuichambua. Wanaotumia nadharia hii katika ufundishaji wa fasihi wanaamini kuwa ni jukumu la mwanafunzi kuweza kuteua vitabu vya fasihi ambavyo angetaka kuvisoma. Kulingana na Njogu na Chimera (2008), mwanafunzi anapaswa kuongozwa tu na wale walio na tajiriba kumliko katika uteuzi wa vitabu vya fasihi. Kwa kumshirikisha mwanafunzi kikamilifu katika uteuzi wa vitabu, hamu yake ya usomaji wa vitabu vyenyewe baada ya uteuzi huimarika kikamilifu.

Wakati mwalimu anafundisha fasihi, anafaa kuwa mwangalifu asijifanye anajua kila kitu. Njogu na Chimera (2008), wanasema kuwa mwalimu anapofundisha fasihi hafai kujifanya kuwa mjuzi wa masuala yote ya fasihi. Badala yake wanapendekeza kuwa mwalimu mwenyewe ajiweke katika hali ya kutojua sana ili awape ruhusa wanafunzi wake waweze kumuonyesha wanayajua yepi na ni yepi ambayo hawajui. Kwa kufanya hivi mwalimu atakuwa amejenga ari ya kutaka kujigundulia mambo miongoni mwa wanafunzi wake wa somo la fasihi.

Mtu hujifunza vyema kwa kuachwa huru kuyatalii mazingira yake. Waasisi wa nadharia hii wanaamini kuwa ili mwanafunzi wa fasihi asome na kuelewa somo vizuri anafaa kuachiwa vitabu vyenyewe ili awe huru anapovisoma na hata kuvichambua. Kwa kufanya hivi mwanafunzi ataweza kupata nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu kazi husika bila ushawishi wa mwalimu. Wanafunzi wanapoachwa peke yao huweza kujiamini na kuwa wakakamavu katika uchambuzi wao.

Spivey kama alivyonukuliwa na Al (2017), anasema kuwa waasisi wa nadharia hii wanapendekeza kuingiliana kwa wanafunzi huku wakisaidiana wao kwa wao katika


shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inawapa fursa wanafunzi kuweza kuingiliana na kusaidiana wakiwa katika makundi wakati wa kutekeleza shughuli husika.

Aidha waasisi wa nadharia hii huhitaji walimu kuwaelekeza wanafunzi ili waweze kuwasilisha kile kinachofundishwa kwa njia mbalimbali (Sadoski na Paivio, 2013). Wakati wa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, wanafunzi huweza kuwasilisha vijimada mbalimbali vya mada kuu mbele ya darasa nzima baada ya kuvizungumzia katika vikundi vidogovidogo wakati wa kutekeleza shughuli.

Nadharia hii itaunufaisha utafiti huu kwa sababu ina mihimili ambayo inasisitiza sana kushirikishwa kwa mwanafunzi kikamilifu katika shughuli ya ujifunzaji na ufundishaji wa fasihi. Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kuwashirikisha wanafunzi kikamilifu kulingana na mazingira yao. Aidha wanafunzi hupewa ruhusa ya kuingiliana wao kwa wao na hivyo basi, kujivumbulia na kujigundulia mambo.

## 1.11 Mgofu Dhanifu wa Utafiti

Hiki ni kielekezo cha dhana inayotafitiwa kinachoonyesha uhusiano wa vigeu huru na vigeu tegemezi katika utafiti. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), mgofu dhanifu wa utafiti husaidia mtafiti kuonyesha uelewaji wake wa swala husika na kuliwasilisha. Humfanya mtafiti kujikita katika suala na kuonyesha uhusiano wa masuala na data ili kudhihirisha undani wa yote mawili.




**Mchoro 1. 1: Mgofu Dhanifu wa Utafiti unaonyesha Vigeu huru, Vigeu ingilizi na Vigeu tegemezi.**

Mchoro huu unabainisha vigeu huru vitatu; mada za riwaya, mitazamo ya walimu na mbinu za kufundishia. Vigeu ingilizi navyo ni pamoja na mazingira ya darasani, uwezo wa kiakili wa wanafunzi, idadi ya vipindi vya fasihi kwa wiki pamoja na vifaa vya kufundishia. Vigeu tegemezi ni viwili ambavyo ni matumizi ya mbinu fasaha katika ufundishaji wa somo la riwaya pamoja na utendaji bora wa wanafunzi katika mtihani. Vigeu hivi viwili vitaweza kuathiriwa na jinsi wanafunzi wanaposhirikishwa katika shughuli nzima ya ujifunzaji na ufundishaji miongoni mwa vigeu vingine.

## 1.12 Ufafanuzi wa Istilahi

| | | |
|---|---|---|
| **Falsafa** | **:** | Mtazamo fulani wa kimaisha. |
| **Fasihi** | **:** | Hii ni sanaa inayotumia maneno ili kueleza kuhusu maisha na tajriba ya binadamu ulimwenguni. |
| **Mbinu inayotegemea Shughuli** | **:** | Njia ya ufundishaji ambapo mwanafunzi hushirikishwa kutenda jambo (task) ambalo linamuwezesha kuelewa somo zaidi |
| **Mtazamo** | **:** | Jinsi mtu anavyoliona jambo. |
| **Riwaya** | **:** | Kazi ya kinathari yenye urefu wa kutosha. |
| **Ubunaji** | **:** | Nadharia inayosisitiza ushirikishwaji wa mwanafunzi katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. |
| **Ufundishaji** | **:** | Kitendo cha kutoa mafunzo ili kuwe kuwaelekeza wanafunzi. |
| **Ujifunzaji** | **:** | Kitendo cha kupokea mafunzo kwa wanafunzi ili waelewe. |
| **Utanzu** | **:** | Tawi la fasihi. |

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia yaliyoandikwa kuhusu ufundishaji wa somo la riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Miongoni mwa yale yaliyoshughulikiwa ni pamoja na ufundishaji wa fasihi, mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi kwa ujumla, mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, ufundishaji wa riwaya, ufaafu wa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na changamoto wanazokabiliana nazo walimu wanapotumia mbinu hii. Mwisho kabisa katika sura hii, mtafiti alijaribu kuonyesha pengo lililopo katika tafiti za awali. Ili kufanikiwa katika shughuli hii, mtafiti aliweza kuonyesha vile ambavyo watafiti wa awali wanavyosema kuhusu mada husika.

## 2.2 Mbinu za Ufundishaji wa Fasihi

Kulingana na TATAKI (2014), Mbinu ni njia ya kutekeleza jambo. Taasisi hii pia inaelezea maana ya ufundishaji kama namna ya kueleza mtu jambo ili alifahamu. Kwa mujibu wa Twoli na Wenzake (2007), mbinu za ufundishaji ni njia zinazotumiwa na mwalimu katika kumuonyesha mwanafunzi jinsi ya kufanya jambo fulani. Wanaelezea zaidi kuwa shughuli hiyo ya kumuonyesha inaweza kuhusisha kumwambia, kumweleza, kumwonyesha au hata kumwelekeza. Kulingana na maelezo haya basi, mbinu za ufundishaji zinaweza kuelezewa kuwa njia mbalimbali zinazotumiwa na mwalimu katika shughuli ya kutoa mafunzo kwa mwanafunzi. Mbinu ya ufundishaji inayotumiwa katika shughuli nzima ya ufundishaji huathiri

uelewaji wa wanafunzi wa kile kinachofundishwa. Kulingana na Twoli na Wenzake (2007), mbinu za ufundishaji zimegawika katika makundi mawili makuu; mbinu zinazomwegemea sana mwalimu na zile zinazoegemea upande wa mwanafunzi. Mbinu zinazomwegemea sana mwalimu ni zile ambazo humshirikisha mwalimu zaidi katika shughuli ya ufundishaji. Mbinu hizi ni kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili.

### 2.2.1 Mbinu zinazomwegemea zaidi Mwanafunzi

Hizi ni mbinu za ufundishaji ambazo humhitaji mwanafunzi kuyafanya mambo mengi katika shughuli za ujifunzaji na ufundishaji. Kulingana na Twoli na Wenzake (2007), mbinu inayomwegemea zaidi mwanafunzi ni mbinu inayomhitaji mwalimu kumsaidia mwanafunzi kufanya uvumbuzi. Wanaelezea zaidi kuwa mwalimu hufanya hivyo kwa kumshirikisha mwanafunzi katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji kwa njia mbalimbali kama vile kumuuliza maswali, kumuelekeza mwanafunzi kule anakoweza kupata habari na pia kumpa maoni yake kuhusu jinsi ya kutatua baadhi ya changamoto anazoweza kukabiliana nazo. Kwa mujibu wa Chang (2010), katika matumizi ya mbinu hizi mwalimu huwa mwelekezi tu na shughuli zote zinazohusu ufundishaji na ujifunzaji humzungukia tu mwanafunzi. Katika uelekezi wake, mwalimu huhitajika kumwasilishia mwanafunzi vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji darasani au popote pale ambapo kipindi kinafanyiwa.

Mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi huwa na uzuri na ubaya wake. Kulingana na Ur (2013), Mwalimu anapotumia mbinu inayomshirikisha mwanafunzi sana katika shughuli nzima ya ufundishaji, ubunifu miongoni mwa wanafunzi wenyewe hujengeka. Hali hii itawafanya wanafunzi waweze

kujivumbulia mambo mapya. Kwa kutumia mbinu zinazotegemea shughuli za wanafunzi, wanafunzi wenyewe wataweza kuelewa vizuri sana na yale ambayo yanafundishwa na walimu wao. Aidha mbinu hizi huwawezesha wanafunzi kuweza kuafikia malengo ya vipindi vinavyofundishwa tena kwa njia yenye urahisi mno. Twoli na Wenzake (2007) wanaendelea kuelezea uzuri wa mbinu hizi zaidi kwa kusema kuwa matumizi yake huwawezesha wanafunzi kuelewa mambo yanayofundishwa kwa undani zaidi. Ur (2013), anaendelea kuelezea kuwa mwalimu anayetumia mbinu zinazotegemea shughuli za mwanafunzi huyagusa maisha ya mwanafunzi wake kwa njia ya kipekee. Mwanafunzi anayeshirikishwa sana katika shughuli ya ufundishaji huweza kuhusisha moja kwa moja yale anayofundishwa darasani na hali halisi ya kimaisha katika ulimwengu nje ya darasa.

Hata hivyo, kulingana na Kulik, Kulik na Carmichael (2016), kuna baadhi ya wanafunzi ambao hawapendi mbinu za ufundishaji ambazo huwashirikisha wao wenyewe katika shughuli ya ufundishaji. Hawa ni wanafunzi ambao kiwango chao cha uelewa ni cha chini. Kulik na Wenzake (2016) wanaelezea zaidi kuwa wanafunzi wa aina hii hufurahia vipindi vinavyofundishwa kwa mbinu zinazomshirikisha zaidi mwalimu katika shughuli za ufundishaji kuliko mwanafunzi. Aidha kulingana na Chang (2010), matumizi ya mbinu hizi huhitaji muda mwingi wa matayarisho wa vipindi vyenyewe kwa upande wa walimu. Pia vipindi vinavyofundishwa kwa kutumia mbinu hizi huchukua muda mrefu hasa ikizingatiwa kuwa wanafunzi huelewa kwa viwango tofauti sana licha ya kuwa katika darasa moja.

Changamoto nyingine ya matumizi ya mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi ni kupotoka kwa wanafunzi hasa pale ambapo uelekezi wa mwalimu umekosekana.

Kupotoka huko kunaweza kuwafanya wanafunzi kujifunza mambo yaliyo nje ya yale wanayofaa kujifunza. Pamoja na hayo, wasomi wengi wanapendekeza kwa kauli moja kuwa mbinu mwafaka zaidi zinazofaa kutumika kwa wingi katika ufundishaji ni zile zinazowashirikisha wanafunzi sana katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Miongoni mwa mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi ni pamoja na mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, ufundishaji marika, mijadala ya darasani na uigizaji.

Kwa hivyo, kwa kuwa watafiti wa awali walipendekeza matumizi ya mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi katika ufundishaji, utafiti huu ulijishughulisha na matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya. Mbinu hii ni miongoni mwa mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi katika shughuli nzima ya ujifunzaji na ufundishaji. Utafiti huu ulitumia tafiti za awali kama msingi wake na mtafiti alichagua kaunti ndogo ya Mukaa kama eneo la utafiti wake kwa kuwa hamna utafiti wa awali uliowahi kufanywa sehemu hiyo hasa kuhusu ufundishaji wa riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

## 2.3 Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Kulingana na Ellis (2003), shughuli ya mwanafunzi ni jambo lolote linalofanywa na mwanafunzi kwa nia ya kuelewa kile kinachofundishwa. Jambo lenyewe linaweza kuhusisha kuchora michoro, majedwali, kusikiliza kanda, kusikiliza maagizo au kufanya vile mwanafunzi anavyotakiwa na mwalimu. Nunan (2006), anaeleza shughuli kama jambo linalowahusisha wanafunzi kuingiliana wakitumia lugha lengwa na wakiwa na nia ya kuimarisha ujuzi wao wa lugha hiyo lengwa kikamilifu. Kwa hivyo, shughuli inaweza kuelezwa kama jambo lolote lile linalofanywa na

wanafunzi chini ya uelekezi wa mwalimu wakiwa na lengo la kujifundisha mambo mapya. Maingiliano ya wanafunzi darasani au hata nje ya darasa katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji huchangia pakubwa katika kuwafundisha wanafunzi mambo husika.

Katika ufundishaji wa riwaya shughuli zenyewe zinahusisha mambo kama vile kusoma kifungu fulani cha riwaya au kusoma hadithi nzima, kuelezea sifa mbalimbali za wahusika, kuchambua maudhui yanayojitokeza katika riwaya husika pamoja na kujadili mbinu za uandishi zilizotumika na mwandishi (Nunan, 2006). Kwa mujibu wa Chetty, Friedman na Rockoff (2014), wanafunzi huhitaji kushirikishwa katika shughuli katika ufundishaji wa riwaya ili kujaza akili zao tupu kwa masuala husika katika riwaya. Mambo wanayosoma wanafunzi wanaposhirikishwa katika shughuli hizo huweka alama katika akili zao ambayo hubaki milele. Kulik na Wenzake (2016), wanaelezea kuwa wanafunzi wa kiwango cha chini cha uelewa wanahitaji kushirikishwa katika shughuli za kusoma na kuchambua riwaya kwa utaratibu mno au polepole sana ili kufuatilia kwa makini shughuli husika ili waweze kupata fursa ya kuuliza maswali kwa undani kuhusu kile wasichokielewa. Tafiti hizi zilitumiwa kama msingi wa utafiti huu kwa kuwa zinazungumzia ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli nzima ya ufundishaji. Utafiti uliofanywa ulihusisha mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji ambayo humshirikisha mwanafunzi zaidi katika shughuli nzima ya ujifunzaji na ufundishaji.

Richard na Rodgers (2014), wanasema kwamba wakati ambapo mwalimu anafundisha mambo rahisi katika riwaya, mwanafunzi anafaa kushirikishwa katika shughuli za kusoma vifungu vya riwaya, kuchambua sifa za wahusika na kueleza

mbinu za uandishi kwa muda mfupi. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi hao wataweza kuelewa masuala husika. Kwa mujibu wa Richards na Renandya (2014), masuala ya kimsingi katika riwaya yanapofundishwa kama vile ploti ya riwaya yenyewe, wanafunzi hushirikishwa katika shughuli za kusoma hadithi wakiwa katika makundi mbalimbali. Wasomi hao wanaelezea zaidi kuwa wanafunzi wanaposhirikishwa katika shughuli za kusoma hadithi huweza kuelewa vipengele vya riwaya vinavyofuatia kwa undani sana. Kulingana na Chetty na Wenzake (2014), katika ufundishaji wa riwaya wanafunzi wanapaswa kupewa shughuli za kuchambua wahusika wakiwa katika makundi na badaaye kuwasilisha kazi yao ya shughuli za makundi darasani. Kila kundi linafaa kupewa mhusika mmoja ili kuweza kuchambua hulka na umuhimu wake katika riwaya husika.

Matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji yana uzuri na ubaya wake kwa wanafunzi na hata walimu ambao wanaitumia mbinu yenyewe. Richards na Renandya (2014), wanasema kuwa matumizi ya shughuli mbalimbali katika ufundishaji yanafanya kile kinachofundishwa kieleweke vizuri. Ni wazi kuwa wanafunzi wanaposhirikishwa katika shughuli katika ufundishaji wa riwaya wataweza kuelewa masuala yanayozungumziwa katika riwaya hiyo kwa undani zaidi. Kwa mujibu wa Richard na Rodgers (2014), wanafunzi wanapojadiliana masuala mbalimbali kuhusu mada inayofundishwa katika utekelezaji wa shughuli, wao wenyewe hufundishana mengi.  Jambo hili huwafanya wanafunzi kuelewa na kujivunia uelewa wao ambao umetokana na shughuli zao wenyewe. Aidha kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji kunaweza kuibua na kukuza vipawa tofautitofauti miongoni mwa wanafunzi kando na kile kinachofundishwa katika kipindi husika.

Kwa mujibu wa Carless (2012), shughuli za wanafunzi za ujifunzaji kwa kawaida hutekelezwa katika makundi. Carless anaelezea zaidi kuwa wanafunzi hujivunia kwa kiwango kikubwa mafunzo yote wanayoyapata wakiwa katika vikundi hivyo kwa kuwa wanaamini ya kwamba mafunzo yenyewe yanatokana na shughuli zao wenyewe.

Mtafiti alizitumia tafiti hizo za awali kama msingi wa utafiti wake. Aidha mtafiti aliweza kuchunguza iwapo matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya huweza hasa kuathiri uelewa wa mwanafunzi wa kile kinachofundishwa. Ili kubainisha hayo mtafiti aliweza kulinganisha matokeo ya mtihani wa wanafunzi waliofundishwa kwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na matokeo ya wanafunzi wao hao walipofundishwa riwaya kwa matumizi ya mbinu za kawaida ambazo hazihuzishi shughuli za mwanafunzi kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili. Kwa kulinganisha matokeo hayo ya mtihani wa wanafunzi, mtafiti aliweza kubaini ukweli kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na jinsi inavyoathiri kwa kiwango kikubwa uelewa wa wanafunzi wa somo la fasihi.

### 2.3.1 Hatua Mbalimbali za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Kulingana na Richards na Renandya (2014), mwalimu anapotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, kipindi huwa na sehemu au hatua mbalimbali. Katika hatua ya kwanza, mwalimu hutanguliza kipindi kwa kuwaelekeza wanafunzi vile angetaka wafanye. Yaani, hii ndio hatua ya kuwapa shughuli yenyewe ambayo angetaka washiriki. Shughuli inaweza kuwa ya aina mbalimbali kutegemea kile kinachofundishwa katika somo husika. Kwa mfano,

iwapo ni somo la fasihi, anaweza kuwapa sura mojawapo katika kitabu cha riwaya waisome au waichambue.

Katika hatua ya pili**,** mwalimu anapaswa kuwagawa wanafunzi katika makundi mbalimbali**.** Richards na Renandya **(**2014**),** wanasema kuwa mwalimu anapowagawanya wanafunzi katika makundi darasani anafaa kuzingatia mambo kadha. Miongoni mwa mambo ya kuzingatiwa ni pamoja na uwezo wa kiakili wa wanafunzi, jinsia ya wanafunzi hasa katika madarasa yaliyo na wanafunzi wa jinsia zote mbili miongoni mwa vigezo vingine. Wanafunzi hufanya au hutekeleza shughuli husika wakiwa katika makundi, wakati huu mwalimu anawaelekeza na kuwapa motisha. Ni jambo la muhimu sana kuwaelekeza wanafunzi wakiwa katika makundi haya ili wasiweze kupotoshana.

Katika hatua ya tatu, wanafunzi wanatakiwa kuandaa ripoti ndogo ya kusoma na kueleza moja kwa moja kilichofanyika wakati wa shughuli. Ripoti hii husomwa na kikundi kimoja baada ya kingine mbele ya wanafunzi wale wengine pamoja na mwalimu darasani. Richards na Renandya (2014), wanasema kuwa, wakati huu kila mwanafunzi ana uhuru wa kuuliza maswali yanayohusu kile ambacho kinawasilishwa ili aweze kuelewa kikamilifu. Wasomi hao wanaongezea zaidi kuwa iwapo kuna maswali ambayo yanawapa changamoto wanafunzi katika kuyajibu, ni vizuri mwalimu kuingilia ili kuweza kutoa maelezo na majibu mwafaka. Rost (2013), anaelezea zaidi kwamba wakati huo mwalimu anapaswa kuwepo ili kuwapa mawaidha wanafunzi na kujibu maswali magumu ambayo wanaweza kuwa nayo kuhusu shughuli waliyoitekeleza.

Katika hatua ya nne, ripoti iliyoandaliwa katika hatua ya tatu hutolewa darasani. Wanafunzi huripoti darasani kwa kutoa hotuba fupi /maelezo mafupi ya kimdomo

au kusoma kuhusu yaliyofanyika wakati wa shughuli husika. Wakati huo mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi rekodi za video za wanafunzi wengine wakifanya shughuli sawa. Rost (2013), anasema kuwa wakati huu mwalimu anapaswa kuwapa wanafunzi hoja zaidi kuhusu mada iliyoshughulikiwa. Aidha wanafunzi wanatakiwa kuuliza, kujibu maswali na hata kunakili hoja muhimu kuhusu walichojadili na kujifunza katika hatua hii. Ni katika hatua hii ambapo mwalimu huwakosoa wanafunzi na kuwapa mwelekeo kuhusu kile kilichofundishwa.

Katika hatua ya mwisho ya kipindi**,** mwalimu huwapa wanafunzi mazoezi kuhusiana na mada husika ili kuimarisha uelewa wao wa somo. Ur (2013), akiandika kuhusu umuhimu wa mazoezi ya ziada katika ufundishaji anasema kwamba, mazoezi humsaidia mwanafunzi kuelewa sehemu ambazo kulingana na mwalimu ni ngumu kiasi kwa mwanafunzi na hazikueleweka na mwanafunzi vizuri wakati wa ufundishaji. Mwanafunzi hutakiwa kuyafanya mazoezi hayo na baadaye kuuliza mwalimu maswali kuhusu sehemu zozote zenye changamoto kwake. Inatarajiwa kuwa kufikia hatua hii, mwanafunzi huwa ameshirikishwa kikamilifu katika somo na kwamba ameweza kuelewa vizuri na kila sehemu ya somo husika. Yaani, malengo ya kipindi yameweza kutimizwa kama yalivyopangwa. Katika utafiti uliofanywa mtafiti aliwaelekeza walimu vyema kuhusu hatua zinazofuatwa katika matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi wakati wa ufundishaji wa riwaya. Kwa kufanya hivyo mtafiti alihakikisha kuwa wanafunzi katika makundi ya utafiti walikuwa wakifundishwa kwa kutumia mbinu iliyokuwa ikitafitiwa na walifundishwa kwa mbinu hiyo jinsi ilivyofaa. Matokeo ya tafiti hizo za awali kuhusu hatua za kufuatwa wakati wa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi yalikuwa msingi imara wa utafiti huu.

### 2.3.2 Sifa za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ina sifa zake bainifu ambazo huitambulisha na kuitofautisha na mbinu zingine za ufundishaji. Baadhi ya sifa hizo zinajadiliwa kwa kina katika sehemu hii.

Rost (2013), anasema kwamba mbinu hii ya ufundishaji ina sifa kadha kama vile kuwashirikisha wanafunzi kikamilifu katika shughuli ya ujifunzaji na ufundishaji. Bila ushiriki wa wanafunzi katika shughuli zinazohuhusu ufundishaji na ujifunzaji hatuwezi kuwepo na mbinu hii. Hali kadhalika mbinu hii inapotumiwa, kazi ya mwalimu huwa imebanwa kwa kiwango kikubwa, yeye huachiwa jukumu la uelekezi tu. Lazima pawepo na shughuli au jambo fulani linalotekelezwa na wanafunzi chini ya uangalizi wa mwalimu.

Aidha, mbinu hii hutumia utaratibu fulani unaozingatiwa katika utekelezaji wa shughuli yenyewe. Utaratibu huu unahusu hatua mbalimbali katika matumizi ya mbinu yenyewe. Kwa mujibu wa Richard na Rodgers (2014), hatua hizi zinapofuatiwa kikamilifu huchangia pakubwa katika kufaulu kwa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji. Matumizi ya mbinu hii hayawezi kukamilika bila kuwepo kwa wanafunzi ambao wamejitolea kushiriki katika kipindi bila kulazimishwa na mwalimu. Chang (2010), anasema kwamba wanafunzi wenyewe wanafaa kuwa na ari ya kushiriki katika kipindi ili kuweza kurahisisha kazi ya mwalimu ya ufundishaji iwapo anatumia mbinu inayomshirikisha mwanafunzi. Anaongezea kuwa iwapo wanafunzi hawana ari ya kushiriki katika kipindi basi kazi ya mwalimu huwa ngumu sana na hali hii huathiri uelewa wa wanafunzi wa kile kinachofundishwa. Kulingana na Kang'ahi (2012), wanafunzi wanapokosa kushiriki katika kipindi kwa kujitolea hufanya kipindi

chenyewe kuchukua muda mrefu huku mwalimu akijaribu kuwashawishi wanafunzi ili waweze kushiriki.

### 2.4 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Walimu wengi wanaamini kwamba mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumika vyema katika ufundishaji huchangia pakubwa katika uelewa wa ndani wa mwanafunzi wa kile kinachofundishwa (Twoli na Wenzake, 2007). Wasomi hawa wanaelezea zaidi kuhusu kuhusika kwa mwanafunzi katika kipindi. Ukweli ni kuwa jinsi mwanafunzi anavyohusika zaidi katika kipindi ndivyo anavyoelewa kwa undani kile ambacho kinafundishwa. Maoni ya walimu ni kuwa wanafunzi wote wanahitaji kushirikishwa katika kipindi kwa kutakiwa kufanya shughuli mbalimbali kutegemea uwezo wa kila mwanafunzi.

Kwa mujibu wa Ellis (2006), walimu wanaotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huamini kuwa mbinu hiyo huwawezesha wanafunzi kubadilishana mawazo na hivyo kufundishana wao kwa wao. Mbinu hii inapotumiwa katika ufundishaji wa riwaya, walimu huamini kwamba itawawezesha wanafunzi kujifunza vipengele vingi zaidi vya riwaya kama vile maudhui, sifa za wahusika, mbinu za wahusika miongoni mwa vingine. Rost (2013), anasema kwamba mwalimu anayetumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huwawezesha wanafunzi wake kuimarisha ujuzi wao wa mazungumzo, mahusiano yao na lugha yao kijumla. Kulingana na Rost (2013), jambo hili huwezekana kwa kuwa wanafunzi hao huingiliana kwa wakati mwingi pale ambapo wanatekeleza shughuli husika.

Hata hivyo, kulingana na Carless (2012), walimu wanafaa kuelewa viwango mbalimbali vya uelewa wa wanafunzi wao. Msomi huyu anaelezea zaidi kuwa

wanafunzi wanaofaa kufundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli ni wale wenye uelewa wa kiwango cha juu. Wanafunzi ambao uelewa wao ni wa chini hawapendi kamwe matumizi ya mbinu hii. Wanafunzi wa aina hii huogopa hasa pale ambapo wanatakiwa kusimama mbele ya wenzao darasani ili kuwasilisha waliyojifunza katika makundi walipokuwa wakitekeleza shughuli husika katika mojawapo wa hatua za kipindi.

Kulingana na Kang'ahi (2012), kuna baadhi ya walimu ingawa wachache ambao huamini kuwa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji huhitaji muda mrefu. Kang'ahi anaelezea zaidi kuwa walimu hao huamini kuwa kipindi ambacho hufundishwa kwa kutumia mbinu hiyo huchukua muda mrefu kukamilika na hivyo basi silabasi hubakia nyuma kwa mwalimu ambaye anaitumia mbinu hio kufundishia fasihi kila wakati. Kulingana na mtazamo wa walimu hao matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi hayahitaji kuwa ya vipindi vyote ili kuweza kuokoa wakati na wakati uo huo kuweza kukamilisha vipindi vilivyopangwa kwa wakati unaofaa. Wanapendekeza kwamba mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi itumike pamoja na mbinu zingine za ufundishaji kwa kutegemea mada inayofundishwa. Kwa mujibu wa Kang'ahi (2012), iwapo mchanganyiko wa mbinu mbalimbali utatumiwa katika ufundishaji wa fasihi huku msisitizo ukiwepo kwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, basi malengo ya ufundishaji wa vipindi mbalimbali vya fasihi yataweza kutimizwa na walimu husika kikamilifu na kwa wakati ufaao.

## 2.5 Ufundishaji wa Riwaya

Osazee (2004), alifanya utafiti wake kuhusu ari na tabia ya usomaji vitabu miongoni mwa waafrika. Kulingana na Osazee (2004), mfumo wa elimu katika bara la Afrika

umejikita katika vitabu vya kiada ambavyo huathiri usomaji wa kujiburudisha. Msomi huyu katika utafiti wake anasema kwamba mfumo huo ndio uliopo nchini Kenya na unawafanya wanafunzi wasiwe na hamu ya kuvisoma vitabu vya fasihi kama vile riwaya. Gramov (2009), anaunga mkono utafiti uliofanywa Nairobi kwa wanafunzi waliomaliza shule za upili. Utafiti huo ulionyesha kuwa mfumo wa elimu unaotakikana kuhimiza ari ya kusoma miongoni mwa wanafunzi haufanyi hivyo.

Wanafunzi hao walitakiwa kutaja vitabu walivyovisoma katika somo la fasihi na walitaja vitabu ambavyo vilikuwa vya kutahiniwa katika mtihani wao wa K.C.S.E. Walipotakiwa pia wataje baadhi ya maudhui katika vitabu hivyo vya kiada hawangeweza. Hii ni ishara kuwa ufundishaji wa riwaya na fasihi kwa ujumla nchini hautimizi malengo yake na unakumbwa na changamoto kadhaa.

Kang'ahi **(**2012**),** anasema ya kwamba katika ufundishaji wa riwaya kunapaswa kuwa na matumizi ya mbinu kadhaa za ufundishaji ili vipindi viweze kuwavutia wanafunzi na wakati huo huo malengo ya ufundishaji yaweze kuafikiwa. Pamoja na hayo, msomi huyo anasisitiza kuwa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi yanapaswa kuwa kwa wingi ikilinganishwa na mbinu zile zingine za ufundishaji. Kang'ahi (2012), anasema kuwa katika ufundishaji wa riwaya, mwanafunzi anapaswa kufanya mambo kadhaa peke yake huku mwalimu akiwa mwelekezi tu. Baadhi ya mambo ambayo yanapaswa kufanywa na wanafunzi ni pamoja na kujisomea vitabu vya hadithi peke yao, kuchambua hadithi pamoja na kuuliza na kujibu maswali husika.

### 2.6 Ufaafu wa Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Mbinu hii ina uzuri wake katika shughuli nzima ya ufundishaji. Kulingana na Rost (2013), mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumika katika

ufundishaji hukuza ubunifu miongoni mwa wanafunzi kwa sababu wako huru kutumia lugha jinsi wawezavyo. Pia, wanafunzi huweza kuhusisha mada na hali halisi ya kimaisha na hivyo basi kuelewa vyema kile kinachofundishwa. Kulingana na Richard na Rodgers (2014), wanafunzi wanapotumia mbinu hii kujifunza, zaidi ya kujifunza fasihi huweza kupata uwanja mpana wa kujifunza mambo mengine kama vile msamiati. Rost (2013), anaongezea kuwa wanafunzi wanaotumia mbinu hii hufurahia na kufuatilia kwa makini yale yanayofanyika na hivyo basi, kuleta ari katika masomo.

Aidha wanafunzi wanapotumia mbinu hii hufundishana mengi wao wenyewe. Rost anaelezea zaidi kuwa mbinu hii ndiyo inayofaa zaidi kutumika kufundushia kwa sababu inachangia pakubwa katika kuelewa kwa wanafunzi na kile kinachofundishwa. Hata hivyo, Rost (2013) hakusahau kutaja kuwa kuna idadi ndogo ya wanafunzi ambao hawafurahii kamwe matumizi ya mbinu hii katika shughuli za ujifunzaji na ufundishaji. Kulingana na msomi huyu hao ni wanafunzi wavivu ambao hutaka kufanyiwa kila kitu na mwalimu na kuachiwa jukumu la kupokea mafunzo tu wakiwa katika hali ya upokezi.

Chang' (2010), anasema kwamba matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi yanaweza kumfanya mwalimu kugundua talanta zilizojificha miongoni mwa wanafunzi wake. Anaelezea kuwa wanafunzi wanaposhiriki katika shughuli na baadaye kuwasilisha ripoti mbele ya hadhira darasani wanapata ukakamavu wa kuongea mbele ya hadhira. Ukakamavu huo unaweza kuwa chanzo cha talanta fulani katika maisha ya wanafunzi husika kama vile utangazaji, uanahabari na kadhalika. Aidha wanafunzi ambao huchaguliwa na wenzao ili kuweza kusimamia makundi nao pia huweza kuimarisha uwezo wao wa uongozi. Jambo hili linaweza kuwa

chanzo cha wanafunzi hao kuwa viongozi katika siku zijazo. Richard na Rodgers (2014), wanaelezea zaidi kuwa ushindani hutokea miongoni mwa makundi mbalimbali ya wanafunzi katika mawasilisho katika darasa linalotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Kwa mujibu wa msomi huyo, ushindani wenyewe huchangia usomaji wa kina miongoni mwa wanafunzi, jambo linalowafanya wanafunzi hao kuelewa barabara kile kinachofundishwa. Chang' (2010), anasema kwamba popote pale ambapo wanafunzi wanashindana katika masomo, kuna uwezekano mkubwa wa wanafunzi husika kusoma kwa kina na kwa mapana ili waweze kushindana kikamilifu.

## 2.7 Changamoto za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Licha ya uzuri wake, mbinu hii pia hukabiliwa na changamoto kadhaa. Kulingana na Richard na Rodgers (2014), katika darasa ambalo ni kubwa, mbinu hii huenda isitumike kwa sababu ya muda mrefu ambao unahitajika ili kuweza kukamilisha hatua zake zote. Muda mwingi utahitajika kwa kuwa ni lazima wanafunzi hao wote wawekwe katika makundi na kila kundi lihakikishwe kuwa linashughulika kikamilifu. Shughuli nzima ya kuwagawanya wanafunzi wengi na kuwashirikisha katika shughuli kikamilifu huenda ikahitaji muda mrefu ambao ni vigumu kupatikana katika muda wa kawaida wa kipindi.

Halikadhalika baadhi ya wanafunzi wanaweza kukosa kushiriki katika makundi na hivyo basi wakakosa kujifunza chochote. Naye Rost (2013), anasema kuwa bila uelekezi wa mwalimu wanafunzi wenyewe wanaweza kupotoshana wanapotumia mbinu hii. Kulingana na Rost (2013), ili mbinu yenyewe ifanikiwe mwalimu anahitaji kuwa karibu ili aweze kuzuia upotoshanaji miongoni mwa wanafunzi. Hali hii huenda ikaongezea mwalimu kazi nyingi zaidi. Rost (2013), anaelezea zaidi

kuwa kuna idadi ndogo ya wanafunzi ambao hawafurahii kufundishwa kwa mbinu inayotumia shughuli za wanafunzi. Msomi huyu anaelezea zaidi kuwa wanafunzi hao hawawezi kuelewa kile kinachofundishwa kwa sababu hawafurahishwi na mbinu inayotumiwa katika ufundishaji.

Chang' (2010), anelezea kuwa wanafunzi ambao uwezo wao wa uelewa uko chini mno huwa hawapendi mbinu za ufundishaji ambazo huwashirikisha sana katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Kulingana na Chang' (2010), wanafunzi wa aina hiyo hupenda tu kupokea yale yanayofundishwa na walimu bila wao kushirikishwa kwa vyovyote vile. Kuwafundisha wanafunzi wa kiwango hicho kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwalimu huwa jambo ngumu mno na matokeo yake ni kutoelewa kwa wanafunzi wenyewe kuhusu kile kinachofundishwa.

## 2.8 Tafiti zilizoandikwa kuhusiana na Mada

Tafiti mbalimbali zimefanywa nchini Kenya kuhusiana na ufundishaji wa fasihi na matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi kama inavyojadiliwa katika sehemu hii.

Gathumbi (1995), alichunguza matokeo ya kimazungumzo katika mazingira ya uwili lugha, hususan mbinu za ufundishaji wa somo la Kiingereza miongoni mwa shule za sekondari nchini Kenya. Mtafiti huyo akitumia mbinu ya uchunzaji aliweza kuchunguza mtagusano kati ya mwalimu na mwanafunzi katika somo la Kiingereza. Utafiti huo ulionyesha kutawala kwa walimu katika mazungumzo kwa kiwango cha asilimia 75 nao wanafunzi wakawa na asilimia 25 katika mtagusano huu. Kulingana naye walimu walihusika kupita kiasi katika shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji darasani, jambo lililoathiri uelewa wa wanafunzi. Utafiti huo ulipendekeza matumizi

ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji ili kuweza kupata matokeo bora. Utafiti huo ulitumika kama msingi wa utafiti huu kwa kuwa unapendekeza matumizi ya mbinu inayochunguzwa na mtafiti.

Kimani (2015), alifanya utafiti kuhusu uhusiano wa mbinu za kufundishia sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi wa sekondari katika kaunti ndogo ya Thika Magharibi. Katika utafiti wake, aligundua kwamba walimu hawajaimarisha mbinu zao za ufundishaji darasani kama inavyostahili. Aidha aligundua kwamba katika mbinu nyingi zinazotumiwa na walimu kufundishia Kiswahili, wao hutawala kipindi na kushiriki zaidi kuliko wanafunzi wenyewe na kwamba vipindi vilivyotegewa Kiswahili vilikuwa vichache. Mtafiti huyo alipendekeza kuongezwa kwa vipindi vya Kiswahili ili walimu wawashirikishe wanafunzi kikamilifu katika uigizaji, mijadala, maigizo na usomaji wa hadithi kwa wingi. Utafiti huo ulikuwa msingi wa utafiti huu uliofanywa kwa sababu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ni miongoni mwa mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi kwa kiwango kikubwa katika shughuli ya ujifunzaji na ufundishaji.

Ngugi (2009), alitafiti kuhusu hali ya fasihi nchini Kenya. Alishughulikia hasa usomaji wa fasihi kwa ujumla. Msomi huyo alichunguza kwa undani sababu zinazowafanya wanafunzi wasipende kusoma vitabu vya fasihi. Kazi yake inatofautiana na hii inayopendekezwa kwa sababu utafiti huu utajikita katika ufundishaji wa riwaya na sio usomaji wa fasihi kwa ujumla. Hata katika ufundishaji wenyewe, utafiti huu utalenga matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Ngungi katika utafiti wake alitambua kuwa wanafunzi wengi huwa hawapendi kusoma vitabu vya fasihi. Utafiti huu ulijikita katika ufundishaji wa riwaya kama utanzu wa fasihi.

Gituku (1990), alifanya utafiti wake kuhusu vipera vya fasihi simulizi na kuchunguza ufundishaji wake pia. Aligusia mbinu ya maigizo kama inavyotumiwa kufundishia vipera hivyo katika shule za msingi. Utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa ulijihusisha na ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za upili. Hata hivyo utafiti huo wa Gituku (1990), ulitoa mwelekeo kiasi kwa utafiti huu. Mbinu ya maigizo iliyotafitiwa na Gituku ni mbinu ambayo inamshirikisha mwanafunzi katika ufundishaji. Utafiti huu nao ulishughulikia mbinu inayotengemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya. Kwa hivyo, kwa kuwa Gituku alijikita katika shule za msingi, utafiti wake kwa kiwango kidogo uliweza kutumika kama msingi wa utafiti huu katika shule za upili.

Eldredge na Butterfield (1986), walifanya utafiti wa utumiaji wa vitabu vya fasihi ya watoto kufundishia usomaji. Kutokana na utafiti Wao waligundua kwamba utumiaji wa vitabu hivyo katika kufundishia kusoma huwa wenye manufaa kwa kujenga mwelekeo ufaao kwa wanafunzi kuihusu fasihi na kuyahusu maisha kwa ujumla. Kwa kiwango fulani utafiti tulioufanya uliweza kutambua iwapo wanafunzi wa shule za upili wanafurahia kusoma vitabu vya fasihi na pia kama vinaathiri mwelekeo wao wa kimaisha. Aidha utafiti huu ulidhamiria kutambua iwapo wanafunzi wanafurahia wanaposhirikishwa katika kusoma riwaya.

Benton na Fox (1985), walishughulikia ufundishaji wa fasihi kwa ujumla hasa miongoni mwa watoto. Walichunguza jinsi ambavyo watoto hupokea tanzu za hadithi na ushairi. Utafiti huo unaufaa utafiti huu kwa kuwa kama walivyofanya utafiti wao Bentox na Fox (1985), utafiti huu pia ulishughulikia ufundishaji wa fasihi. Hata hivyo, tofauti na utafiti wa Benton na Fox, utafiti huu uliangazia ufundishaji wa fasihi andishi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Aidha

utafiti huu ulijikita katika ufundishaji wa utanzu mmoja wa fasihi andishi kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na sio mbinu zote kwa ujumla.

Odaga (1985), alishughulikia suala la ufundishaji wa fasihi kwa vijana. Katika utafiti wake alifafanua kwamba mchango wa walimu ni muhimu katika ufundishaji wa fasihi ya vijana. Alikariri kwamba walimu wa shule wajishughulishe katika kujenga mwelekeo ufaao ndipo kwanza kuwe na mabadiliko katika hali ya usomaji. Utafiti huo ulisaidia utafiti wa sasa kwa kuwa mtafiti alijaribu kujenga mwelekeo ufaao wa wanafunzi kuhusu usomaji na ufundishaji wa fasihi kwa kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli ya usomaji wa fasihi yenyewe.

Mangeni (2010), alifanya utafiti kuhusu mawasiliano ya kimazungumzo miongoni mwa wanafunzi katika somo la Kiingereza wilayani Kipkelion. Matokeo yake yalikuwa kutawala kwa walimu katika vipindi vyote vya Kiingereza. Kulingana naye, ufundishaji wa aina hii ulichangia katika matokeo mabaya ya wanafunzi baada ya kufanya mtihani. Hili lilikuwa dhihirisho kuwa wengi wa wanfunzi hawakuelewa vyema mada walizofundishwa kutokana na mbinu mbaya za ufundishaji zilizotumiwa na walimu katika eneo hilo. Utafiti uliofanywa ulichunguza uelewa wa wanafunzi wanapofundishwa kwa kutumia mbinu inayowashirikisha wao wenyewe katika ufundishaji.

## 2.9 Pengo la Utafiti

Baada ya kuvipitia vitabu na tasnifu mbalimbali za watafiti tofauti tofauti, ni wazi kuwa tafiti za awali zilishughulikia ufundishaji wa fasihi kwa ujumla katika maeneo mbalimbali. Kimani (2015) akifanya utafiti kuhusu mbinu za kufundishia katika kaunti ndogo ya Thika magharibi, aligundua kuwa wengi wa walimu hawakuwa

wameimarisha mbinu zao za ufundishaji darasani. Utafiti wake ulishughulikia mbinu za ufundishaji Kiswahili kwa ujumla na wala sio mbinu moja mahususi. Ngugi (2009) alifanya utafiti kuhusu usomaji na ufundishaji wa fasihi kwa ujumla miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili nchini Kenya. Katika utafiti wake aligundua kuwa wanafunzi wengi wa somo la fasihi hawakuwa na hamu ya somo lenyewe. Yu (2008) alifanya utafiti wake kuhusu matumizi ya mbinu mbalimbali za kimakundi katika ufundishaji wa fasihi nchini Taiwani. Katika utafiti wake alishughulikia tu jinsi mbinu mbalimbali za kimakundi zinavyotumiwa kufundishia fasihi. Kwa kuwa watafiti hao hawakufanya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya katika eneo la Mukaa, utafiti huu ulifanywa katika eneo hilo. Tafiti hizo za awali zilitumika kama msingi wa utafiti huu. Aidha utafiti huu ulifanyika katika maeneo tofauti kabisa na ya tafiti za awali na ulijihusisha na mbinu moja mahususi ya ufundishaji wa riwaya tofauti kabisa na tafiti hizo za awali.

# SURA YA TATU

# MUUNDO NA MBINU ZA KUKUSANYA DATA

## 3.1 Utangulizi

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya katika shule za upili. Katika sura hii mtafiti alielezea muundo wa utafiti, vigeu vya utafiti, eneo la utafiti, watafitiwa lengwa, mchakato wa kuteua sampuli, mbinu na vifaa vya utafiti majaribio ya vifaa vya utafiti, ukusanyaji, uchanganuzi, uwasilishaji wa data pamoja na maadili ya utafiti.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Creswell (2013), muundo wa utafiti ni utaratibu na mpangilio maalumu wa kukusanya na kuchanganua data. Utafiti huu uliongozwa na muundo wa kimaelezo. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), utafiti wa kimaelezo unaweza kutumika kufafanua mielekeo ya watu, maoni na tabia zao au kuelezea maswala ya kielimu na kijamii. Mtafiti anaamini kuwa muundo huu ulikuwa mwafaka kwa utafiti huu kwa sababu ulimsaidia kujua mbinu zinazotumiwa na waalimu kufundishia riwaya, kuelewa namna walimu wanavyotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi pamoja na kutambua mitazamo na changamoto wanazokabiliana nazo. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa ulitumia uchanganuzi wa kithamani kuchambua vigezo muhimu vya utafiti na kuimarisha matokeo ya data kwa kutumia uchanganuzi wa kiidadi.

### 3.3 Vigeu vya Utafiti

Utafiti huu ulihusisha vigeu huru, vigeu ingilizi na vigeu tegemezi. Katika utafiti wowote ule ambao unatarajiwa kuwa na matokeo ya kweli ambayo yanaweza kutumainiwa, vigeu hivi huwa ni muhimu sana. Vigeu huru katika utafiti huu ni vitatu navyo ni malengo ya silabasi, mitazamo ya walimu na mbinu za ufundishaji. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), vigeu huru huathiri vigeu tegemezi. Vigeu tegemezi katika utafiti huu ni matumizi ya mbinu fasaha katika ufundishaji wa riwaya na utendaji bora wa wanafunzi katika mitihani ya fasihi. Utafiti huu ulichunguza iwapo matumizi ya mbinu ya ufundishaji inayotegemea shughuli za mwanafunzi huathiri utendaji bora wa wanafunzi katika mitihani ya fasihi.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kaunti-ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni nchini Kenya. Kaunti-ndogo ya Mukaa ni miongoni mwa Kaunti-ndogo tisa katika kaunti ya Makueni. Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu ya kuonyesha matokeo ya kiwango cha chini ya wastani katika mtihani wa KCSE karatasi ya Kiswahili katika kipindi cha miaka ya 2014-2017. Aidha, eneo hili lina aina tatu za shule zipatikanazo katika maeneo mengi nchini Kenya; Shule za kitaifa, za kaunti na za kaunti ndogo. Kuwepo kwa mchanganyiko huu wa aina za shule kulimwezesha mtafiti kuibuka na matokeo yanayoweza kutegemewa kuhusu swala la utafiti.

Hali kadhalika katika eneo hili hakuna utafiti wowote ujulikanao na mtafiti kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya katika shule za upili uliowahi kufanywa. Aidha, maeneo ya shule hizi yaliweza kufikiwa kwa urahisi kama asemavyo Singleton alivyonukuliwa na Kimani (2015), maeneo mwafaka ya utafiti yanapaswa kuwa na uhusiano na swala la utafiti,

yaweze kufikiwa kwa urahisi na watafitiwa katika eneo lenyewe waweze kuingiliana vyema na mtafiti. Maoni haya pia yanaungwa mkono na Kemper, Stringfield na Teddlie (2003).

### 3.5 Watafitiwa Lengwa

Watafitiwa ni jumla ya wahusika ambao wanatumiwa ili kupata data ya utafiti. Kwa mujibu wa Sedlock kama anavyonukuliwa na Kimani (2015), watafitiwa ni lazima wafahamike kimaudhui na kiwango. Watafitiwa lengwa katika utafiti huu walikuwa walimu 60 na wanafunzi 2580 katika kaunti-ndogo ya Mukaa. Eneo hili lina shule za Sekondari 43. Walimu waliolengwa ni wale tu wanaofundisha fasihi katika kidato cha tatu katika shule zote za upili. Wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili hawakushirikishwa katika utafiti huu kwa kuwa hawafundishwi fasihi andishi. Pia wanafunzi hao wanachukuliwa kuwa hawana ujuzi wa kutosha wa fasihi andishi. Wanafunzi wa kidato cha nne licha ya kufundishwa fasihi andishi na kuwa na ujuzi wa kutosha, hawakushirikishwa kwenye utafiti kwa sababu walikuwa wakijitayarisha kwa mtihani wa kitaifa wa KCSE.

Wanafunzi wa kidato cha tatu ndio walioshirikishwa katika utafiti huu. Wanafunzi hao wanafundishwa fasihi andishi na kama wenzao wa kidato cha nne wamekuwa katika shule ya sekondari kwa miaka kadha. Mtafiti anaamini kuwa wanafunzi hao wanaelewa masuala yanayohusu usomaji na ujifunzaji wa riwaya. Kwa kuwalenga pia walimu wa fasihi pekee, inaaminika kwamba hao ndio wenye ujuzi kuhusu ufundishaji wa riwaya. Aidha walimu hao ni muhimu zaidi kwa sababu ndio wanaotumia mbinu mbalimbali katika kufundisha riwaya na fasihi kwa ujumla.

### 3.6 Sampuli na Mchakato wa kuteua Sampuli

Kulingana na Sharman kama alivyonukuliwa na Kimani (2015), sampuli ni sehemu ndogo ya vitu au watu wanaotafitiwa ili kudhihirisha sifa sawa za idadi ya vitu au watu wanaowakilishwa ili kupata matokeo yanayoweza kuaminika na kuthibitika. Mbinu mbili zilitumiwa kuteua sampuli. Kwanza, mbinu makusudi ilitumiwa kuzigawa shule zote katika makundi matatu: Shule za kitaifa shule za kaunti na shule za kaunti ndogo. Mbinu hii ilitumiwa ili kuweza kupata sampuli yenye wakilisho la kila aina ya shule. Hii ni kwa sababu shule hizi hutofautiana kwa misingi ya vifaa vya ufundishaji, nyenzo za ufundishaji na hata idadi ya walimu na wanafunzi. Pili, mbinu ya kinasibu ilitumiwa ili kupata shule mbili kutoka katika kila kundi. Jumla ya shule sita zilishirikishwa katika utafiti huu.

Walimu waliteuliwa kwa kutumia mbinu makusudi, walimu wawili kutoka katika kila shule. Jumla ya walimu waliohusika katika utafiti huu walikuwa kumi na wawili. Suala la uana pia lilitiliwa manaani katika kuwateua walimu. Wanafunzi wa madarasa mawili katika kila shule waliteuliwa huku kila darasa likiwa na takribani wanafunzi arobaini na watano. Jumla ya wanafunzi mia tano na arobaini walihusika katika utafiti huu. Mbinu makusudi ilitumika kuwateua wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka katika kila shule. Kwa jumla watafitiwa 552 wakiwemo wanafunzi na walimu walishirikishwa katika utafiti huu, hii ikiwa ni asilimia 19 ya idadi lengwa. Kulingana na Ari na Wenzake kama walivyonukuliwa na Miima (2014), sampuli ya utafiti ya kati ya asilimia 10 – 20 ya idadi lengwa inafaa kwa utafiti wowote ule. Jedwali 3.1 linaonyesha uteuzi wa sampuli.

**Jedwali 3. 1: Uteuzi wa Sampuli**

| SAMPULI | IDADI LENGWA | IDADI MAHUSUSI | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|
| **SHULE** | 43 | 6 | 13.9 |
| **WALIMU** | 60 | 12 | 20 |
| **WANAFUNZI** | 2850 | 540 | 18.9 |
| **JUMLA** | **2910** | **552** | **19** |

### 3.7 Mbinu na Vifaa vya Utafiti

Katika utafiti huu, data ilikusanywa kwa kuzingatia vifaa vinne vifuatavyo; hojaji na mahojiano kwa walimu, mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti na uchunzaji wa somo darasani. Matumizi ya vifaa kadha vya utafiti yalitarajiwa kuwezesha kupata matokeo ambayo yangeweza kutegemewa katika utafiti. Mugenda na Mugenda (2003), wanasisitiza kuwa mtafiti akitumia vifaa mbalimbali hupata matokeo ambayo yanaweza kutegemewa zaidi. Vifaa hivyo vilitumiwa kwa walimu na wanafunzi ambao waliteuliwa.

#### 3.7.1 Hojaji kwa Walimu

Ili kupata habari zisizoweza kupatikana kwa matumizi ya mahojiano au uchunzaji, hojaji zilitumiwa. Kulingana na Wamitila (2003), hojaji ni hati yenye orodha ya maswali ambayo humwongoza mtafiti katika utafiti wake. Hojaji hizo zilishirikisha maswali huru na funge. Kulingana na Nardi (2018), manufaa ya kutumia maswali huru na funge ni kwamba aina moja ya maswali hufidia upungufu wa aina ile nyingine. Hojaji ziliwasilishwa kwa walimu sita wa fasihi andishi walioteuliwa. Umuhimu wake ulikuwa kupata habari za kibinafsi kuwahusu walimu waliohusika, mbinu wanazotumia katika kufundishia riwaya ya Kiswahili, mitazamo yao kuhusu

mbinu inayotafitiwa na changamoto zozote wanazokabiliana nazo wakati wa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

### 3.7.2 Mahojiano

Wamitila (2003), anaeleza mahojiano kama maswali yanayoulizwa na mtafiti ambayo yanajibiwa na mhojiwa. Mpangilio wa mahojiano ulitarajiwa kupata habari kutoka kwa walimu walioteuliwa. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), mahojiano yanamwezesha msaili kujiweka katika hali halisi ya msailiwa na hivyo kupata data bora zaidi. Mugenda na Mugenda wanaeleza zaidi kuwa mahojiano ni bora kuliko hojaji katika kukusanya data. Mtafiti aliwasiliana na walimu walioteuliwa ili kupata data ambayo ilikuwa vigumu kuipata kupitia kwa hojaji. Mahojiano yaliweza kupata data kuhusu madhumuni ya utafiti karibu yote na kuongezea data zilizokusanywa kupitia kwa vifaa vingine vya utafiti. Aidha, mahojiano yalimwezesha mtafiti kupambanua maswali ya utafiti yenye utata ili kumwezesha msailiwa kutoa majibu sahihi na yenye uwazi. Walimu walihojiwa kwa kutumia mahojiano ya maswali-funge na mahojiano ya maswali-huru. Hili lilimwezesha mtafiti kulinganisha majibu hayo na yale ya hojaji na pia yale aliyoyaona darasani.

### 3.7.3 Mtihani wa Mwanzoni na Mwishoni mwa Utafiti

Katika shule mbili teule, kulikuwa na madarasa mawili ya wanafunzi. Wanafunzi wa madarasa yote mawili walihusishwa katika mtihani wa mwanzoni mwa utafiti. Mtihani huo wa mwanzoni ulikuwa na maswali mawili huku kila swali likiwa na alama ishirini. Ulihusu sifa za wahusika na maudhui ya mwandishi katika Riwaya ya Chozi la Heri. Mtihani huu ulidhamiria kutambua kiwango cha uelewa wa

wanafunzi kabla ya kufundishwa kwa mbinu tofauti. Matokeo ya mtihani huu yalilinganishwa kwa makundi yote mawili. Baadaye darasa moja lilifundishwa kipengee cha mbinu zilizotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huku darasa la pili likifundishwa kipengee hicho hicho kwa kutumia mbinu za kawaida za ufundishaji. Hatimaye madarasa yote mawili yalihusishwa katika mtihani wa mwishoni mwa utafiti. Mtihani wa mwishoni mwa utafiti ulikuwa na maswali mawili pia na kila swali lilikuwa na alama ishirini. Swali la kwanza lilihusu mbinu ya kinaya kama ilivyotumiwa na mwandishi wa Chozi la Heri nalo swali la pili lilihusu mbinu ya majazi. Mitihani yote miwili, wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti ilifanywa kwa muda wa saa moja kila mmoja. Mitihani hiyo ilisahihishwa na mtahini wa K.N.E.C. Matokeo ya mtihani wa pili yalilinganishwa pia kwa makundi yote mawili ya wanafunzi.

Haya yalifanyika ili kuweza kupata data kuhusu uelewa wa riwaya kwa matumizi ya mbinu tofauti tofauti za ufundishaji. Data kutokana na mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti zilitumika kutoa majibu kwa madhumuni ya tatu (3) ya utafiti ambayo ni kuchunguza athari ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumiwa kufundishia riwaya kwa utendaji wa wanafunzi.

### 3.7.4 Mwongozo wa Uchunzaji

Mwongozo huu ulitumika kutazama walimu wa fasihi wakifundisha riwaya ya Kiswahili darasani. Mbinu walizotumia katika ufundishaji wao ziliweza kutambuliwa na mtafiti pamoja na baadhi ya changamoto walizokumbana nazo wakitumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa somo la riwaya ya Kiswahili. Aidha kupitia kwa uchunzaji mtafiti aliweza

kuchunguza kiwango cha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanfunzi miongoni mwa walimu katika ufundishaji wa somo la riwaya. Data kutokana na uchunzaji iliweza kunakiliwa na kuchanganuliwa baadaye. Data kutokana na uchunzaji ilitarajiwa kujibu madhumuni yafuatayo ya utafiti: (1) kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa fasihi kufundishia riwaya na (2) kuchunguza ni kwa kiwango kipi walimu wa fasihi wanatumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia somo la riwaya.

### 3.8 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio ya nyanjani kabla ya kuvitumia ili kuhakikisha uhalali na ufaafu wavyo. Kulingana na Orodho (2003), majaribio ya vifaa vya utafiti hufanywa ili kuweza kueleza masuala ambayo huenda hayaeleweki kwa watafiti wakati wa utafiti wenyewe. Katika utafiti huu majaribio ya utafiti yalifanywa katika shule mbili za upili za mseto katika kaunti ndogo ya Mukaa. Shule hizo mbili zilichanguliwa kwa njia ya kinasibu na hazikuhusishwa kamwe katika utafiti halisi. Majaribio hayo yalifanywa kwa walimu 2 na wanafunzi 32. Jumla ya watafitiwa 34 walihusishwa katika majaribio haya ya utafiti. Walimu hao 2 walipewa hojaji za kujaza, walishirikishwa katika mahojiano na mtafiti akashiriki katika uchunzaji darasani wakati walimu hao walipokuwa wakifundisha wanafunzi wao somo la riwaya. Kwa kufanya hivyo mtafiti aliweza kurekebisha baadhi ya sehemu za vifaa vya utafiti zilizokuwa na utata kwa watafitiwa. Aidha mtafiti aliweza kuelewa kuwa kulikuwa na haja ya kufafanua umuhimu wa utafiti kwa wahojiwa pamoja na suala la kuhifadhi data iliyokusanywa kwa siri mno na kuitumia kwa madhumuni ya utafiti pekee. Mtafiti alielewa kuwa kwa kutozingatia

suala hilo watafitiwa hawangekuwa huru kushiriki katika utafiti kama ilivyodhihirika wakati wa majaribio ya utafiti.

Walimu walielekezwa jinsi ya kufundisha kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi baada ya mtafiti kufanya uchunzaji darasani. Aidha wanafunzi waligawanywa katika makundi mawili. Walimu walitakiwa kufundisha kundi moja vipengee vya riwaya wakitumia mbinu iliyokuwa ikitafitiwa na kundi la pili la wanafunzi kwa kutumia mbinu za kawaida za ufundishaji. Hatimaye makundi yote mawili ya wanafunzi yalipewa mtihani wa mwishoni mwa utafiti na matokeo ya mtihani huu kulinganishwa na matokeo ya mtihani wa mwanzoni uliokuwa umepeanwa mwanzoni mwa utafiti. Sehemu za maswali ya mtihani zilizokuwa na utata ziliweza kurekebishwa.

### 3.8.1 Uhalali wa Vifaa vya Utafiti

Kulingana na Orodho (2009), uhalali ni kiwango ambacho vifaa vya utafiti vinatumika inavyofaa. Nao Kombo na Tromp (2006) wanasema uhalali wa vifaa ni kipimo cha kuhakikisha ufaafu na utendakazi wake. Ili kuhakikisha uhalali wa vifaa vya utafiti vikiwemo; mwongozo wa uchunzaji darasani, hojaji, maswali ya mahojiano, mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti, mambo kadha yalizingatiwa. Mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti ulitungwa na mtafiti mwenyewe ambaye ni mwalimu aliyehitimu katika utunzi wa mitihani ya K.C.S.E ya fasihi ya Kiswahili. Mitihani hiyo ilizingatia sheria za utunzi wa mitihani ya K.N.E.C kwa kutahini vipengele ambavyo vinatahiniwa katika mitihani ya fasihi ya kitaifa. Mtihani wa mwanzoni ulitathmini vipengele vya sifa za wahusika na maudhui ya riwaya ya Chozi la Heri huku mtihani wa mwishoni ukitathmini mbinu za uandishi zilizotumika na mwandishi wa riwaya hiyo hiyo.

Kuhusu mwongozo wa uchunzaji wa darasani, hojaji na maswali ya mahojiano, mtafiti alitumia wataalam wawili katika maswala husika kukadiria uhalali wa vifaa hivyo baada ya mtafiti kuvitunga yeye mwenyewe. Mtaalamu mmoja aliulizwa kuweza kutaja kile kilichokuwa kinapimwa na kifaa fulani naye mtaalamu wa pili akitakiwa kutaja mkusanyiko wa vifaa vinavyotumiwa kupimia kipengee fulani. Matokeo yote yalilinganishwa. Vifaa vyote vya utafiti viliweza kuwasilishwa kwa wasimamizi wa mtafiti na kuidhinishwa. Haya yote yalifanywa ili kuhakikisha uhalali wa vifaa vya utafiti. Kwa mujibu wa Rubio na Wenzake (2003) ni muhimu kuzingatia uhalali wa vifaa ili kuhakikisha kuwa vifaa vyenyewe vina utendakazi ufaao na vinatumika vile inavyostahili.

### 3.8.2 Utumainifu wa Vifaa vya Utafiti

Utumainifu wa vifaa vya utafiti ni kiasi ambacho vifaa hivyo vinaweza kuleta matokeo yale yale vinapotumiwa mara kadha (Orodho, 2009). Iwapo maswali ya mtafiti hayaeleweki vizuri na watafitiwa na pia watafitiwa wenyewe wana mwegemeo fulani katika utafiti, mambo haya na mengine mengi huweza kusababisha makosa katika utafiti na hivyo basi kupunguza utumainifu wa utafiti wenyewe (Kimberlein & Winterstein 2008). Ili kupunguza makosa yoyote ambayo yangefanya utafiti ukose utumainifu, mtafiti alifanya mambo kadha. Kwanza, mtafiti alihakikisha kwamba maswali yote katika vifaa vya utafiti yalitumia lugha rahisi ambayo ilieleweka kwa urahisi na watafitiwa. Maswali ambayo yangezua utata wa uelewa hayakuwepo katika vifaa vya utafiti. Aidha maagizo yote katika vifaa vya utafiti hasa katika hojaji yalikuwa wazi kiasi cha kueleweka kwa urahisi na watafitiwa.

Aidha, utumainifu wa vifaa vya utafiti ulisisitizwa zaidi kwa vifaa kufanyiwa majaribio radidi. Yaani, majaribio hayo yalifanywa kwa kurudiwarudiwa katika shule moja teule ya majaribio huku kukiwa na kipindi cha juma moja kati ya majaribio ya kwanza na ya pili. Vifaa vilivyofanyiwa majaribio radidi ni pamoja na mahojiano, hojaji na mtihani wa mwanzoni na wa mwishoni mwa utafiti. Alama kutoka kwa vipindi vyote vya majaribio zililinganishwa kwa kutumia vipimo vya "coefficient" na kupata alama ya utumainifu ya 0.8. Utafiti huu ulichukuliwa kuwa na utumainifu wa kutosha.

### 3.9 Utaratibu wa kukusanya Data

Katika harakati za maandalizi ya utafiti, mtafiti alipata stakabadhi rasmi ya kumruhusu kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mtafiti akitumia barua kutoka chuoni aliomba idhini rasmi ya kufanya utafiti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI). Akiwa amejihami na kibali cha utafiti kutoka kwa tume hiyo, mtafiti alitembelea ofisi za mkuu wa kaunti ya Makueni pamoja na mkurugenzi wa elimu katika kaunti hiyo. Kutoka kwa ofisi hizo mbili mtafiti alipewa barua za kumruhusu kutembelea shule lengwa za upili katika kaunti ndogo ya Mukaa ili kukusanya data kuhusiana na utafiti wake. Baadaye mtafiti alizuru shule hizo teule ili kujifahamisha na kupata kibali kutoka kwa walimu wakuu. Mtafiti pia alikutana na walimu wa fasihi ili kuwaeleza azma yake ya kufanya utafiti katika shule zao. Aidha, walimu walielezwa kuwa data ambazo zingekusanywa zingetumiwa kwa madhumuni ya utafiti pekee na zingehifadhiwa kwa siri mno.

Siku ya kwanza, mtafiti kwa ushirikiano na walimu alizuru madarasa ya wanafunzi wakati walimu wao wakifundisha riwaya ya Chozi la Heri. Kwa kufanya hivyo,

mtafiti aliweza kubainisha mbinu zilizotumiwa na walimu wa fasihi katika kufundisha riwaya ya Chozi la Heri. Aidha mtafiti aliyapatia makundi yote ya utafiti katika shule mbili teule mtihani kuhusu sifa za wahusika na maudhui katika riwaya ya chozi la heri. Baadaye mtafiti alizungumza na kuelewana na walimu hao ili kufundisha wanafunzi kuhusu mbinu za uandishi katika riwaya ya Chozi la Heri. Wanafunzi wa darasa moja katika kila shule walifundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Walimu hao pia walifundisha wanafunzi wa kundi la pili kipengele hicho lakini kwa kutumia mbinu zao za kawaida kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili. Shughuli hii ya ufundishaji iliendelea kwa kipindi cha mwezi mmoja.

Zoezi la ufundishaji likiendelea, mtafiti aliweza kuzuru madarasa ya wanafunzi ili kutazama moja kwa moja ufundishaji ukiendelea. Jambo hili lilifanywa ili kuhakikisha kuwa walimu walitumia mbinu zilizopendekezwa katika ufundishaji wa kila kundi la wanafunzi. Baadaye, mtafiti aliwahoji walimu akitumia maswali teule. Mtafiti aliwauliza walimu ili wajaze hojaji. Hatimaye baada ya ufundishaji kukamilika, mtafiti aliyapa makundi yote mawili ya utafiti mtihani wa pili. Mtihani wa pili ulihusu mbinu za uandishi katika riwaya ya Chozi la Heri. Mtafiti alitathmini mitihani yote miwili.

### 3.10 Uchanganuzi wa Data

Katika utafiti huu, mbinu za uchanganuzi wa data za kiidadi na kithamani zilitumiwa kwa kutegemea madhumuni ya utafiti wenyewe. Data iliyotumika kutathmini madhumuni ya (1), (2), (4) na (5) ambayo ilikusanywa kwa kutumia vifaa vitatu; hojaji, uchunzaji na mahojiano ilipangwa wazi katika makundi ya fikra na dhana zilizolingana kwa kutumia mfumo wa tarakilishi wa “SPSS”. Uchanganuzi

wa kimaelezo ulitumika kuchanganua baadhi ya data kutokana na vifaa hivyo. Kulingana na Valsiner na Rosa (2007) uchanganuzi wa kimaelezo unafaa zaidi kwa kuchanganua data iliyokusanywa kwa njia ya maneno kutoka kwa watafitiwa. Aidha tarakimu elezi kama vile; asilimia, majedwali, chati na grafu zilitumika kuchanganua data hiyo pia.

Data kutokana na mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti ambayo ilitumika kutathmini madhumuni ya (3) ya utafiti huu ilichanganuliwa pia. Matokeo ya mtihani kati ya makundi mawili yalikokotolewa na kulinganishwa kwa kutumia kiunzi cha "t-test" pamoja na ulinganisho wa "ANOVA". Uchanganuzi wa data zingine za utafiti zilizotokana na hojaji na uchunzaji darasani ulifanywa kwa kutumia maelezo.

### 3.11 Uwasilishaji wa Data

Baada ya data kuchanganuliwa kwa njia zilizoelezewa, iliwasilishwa pia kwa njia ya majedwali na michoro mahususi. Aidha maelezo wazi yalitolewa baada ya kila jedwali na mchoro ili kutoa ufafanuzi wenye kueleweka kwa njia ya wazi na kwa undani zaidi. Haya yote yalifanywa ili kuzipa maana data zilizokusanywa na kuchanganuliwa.

### 3.12 Maadili katika Utafiti

Baada ya mtafiti kupata stakabadhi ya kumtambulisha kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, alipata pia cheti cha kumruhusu kufanya utafiti kutoka katika tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI). Aidha, mtafiti alipata barua za idhini ya kutembelea shule mbalimbali katika kaunti ya Makueni kutoka ofisi za mkurugenzi wa elimu na mkuu wa Kaunti, Makueni. Mtafiti alizuru shule zilizofanyiwa utafiti na kujitambulisha kwa walimu wakuu. Aliwaeleza azma yake

ya kufanya utafiti na kuwahakikishia kuwa data na matokeo ya utafiti huo yangetumika tu kwa minajili ya utafiti uliokusudiwa na kuwa yangehifadhiwa kwa siri. Aidha aliwaeleza pia kuhusu umuhimu wa utafiti. Haya yote yalilenga kujenga uaminifu na uwazi kati ya mtafiti na wasailiwa. Mtafiti anaamini kwamba, kwa kuzingatia hayo yote alitoa nafasi kwa wasailiwa kushiriki katika utafiti kwa hiari bila kushurutishwa.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI WA DATA, UCHANGANUZI NA MAJADILIANO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia uwasilishaji wa data, uchanganuzi na majadiliano ya utafiti huu, kulingana na madhumuni ya utafiti wenyewe. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza namna mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi inavyotumiwa kufundisha riwaya ya Kiswahili katika kaunti – ndogo ya Mukaa, Kaunti ya Makueni. Sura hii ina sehemu sita; sehemu ya kwanza inashughulikia urejeshaji wa vifaa vya utafiti na usuli wa wahojiwa. Sehemu ya pili inawasilisha matokeo kuhusu mbinu zinazotumiwa na walimu wa fasihi kufundidhia riwaya. Nayo sehemu ya tatu inawasilisha data kuhusu kiwango ambacho walimu wa fasihi hutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Haya yakiwa ni madhumuni ya pili ya utafiti. Sehemu ya nne ina data kuhusu athari za mbinu husika katika utendaji wa wanafunzi huku sehemu ya tano ikiwasilisha data ya mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotafitiwa. Sehemu ya mwisho inawasilisha data kuhusu changamoto za walimu wanapotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika kufundisha riwaya ya Kiswahili.

### 4.2 Ujumla wa Data na Usuli wa Wahojiwa

Sehemu hii inashughulikia kiwango cha urejeshaji wa vifaa vya utafiti pamoja na sifa za usuli wa wahojiwa.

#### 4.2.1 Kiwango cha Urejeshaji wa Vifaa vya Utafiti

Baada ya vifaa vya utafiti kusambazwa kwa wahojiwa vilirejeshwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4. 1: Kiwango cha Urejeshaji wa Vifaa vya Utafiti**

| **Kifaa** | **Idadi iliyosambazwa** | **Idadi iliyorejeshwa** | **Alisimia (%)** |
|---|---|---|---|
| Hojaji | 12 | 10 | 83 |
| Makala za uchunzaji | 6 | 6 | 100 |
| Mahojiano | 12 | 12 | 100 |
| Mitihani | 540 | 535 | 99 |

Baada ya kuzambazwa kwa vifaa vyote vya utafiti, kwa ujumla kiwango cha urejeshaji kilikuwa asilimia 95.5. Kwa mujibu wa Saunders (2009), kiwango cha urejeshaji wa vifaa vya utafiti cha 50% kinaridhisha, cha 60% ni kizuri na cha 70% ni kizuri mno. Kwa hivyo kiwango hiki cha urejeshaji wa vifaa vya utafiti kilionekana kuwa kizuri mno na mtafiti aliamini kuwa vifaa vilivyorejeshwa vingeweza kutoa data iliyokusudiwa.

#### 4.2.2 Usuli wa Wahojiwa

Katika utafiti wowote ule ni muhimu kutambua usuli wa wahojiwa. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003), Kothari (2004) na Orodho (2003), usuli wa wahojiwa hutoa matokeo yanayoweza kutegemewa kwa kukipa kila kipengele uhalisia

unaofaa. Matokeo ya aina hii yanaweza kulinganishwa na idadi nzima ya watu kwa sababu sifa za sampuli iliyotumika ni kielelezo mwafaka cha idadi hiyo.


Kwanza, utafiti huu uliweza kutambua aina za shule ambako wahojiwa walitoka wakiwemo walimu na wanafunzi. Jedwali lifuatalo linaonyesha aina za shule zilizoshirikishwa katika utafiti huu.

**Jedwali 4. 2: Aina ya Shule Zilizoshirikishwa kwenye Utafiti huu**

| AINA YA SHULE | WANAFUNZI | | WALIMU | |
|---|---|---|---|---|
| | IDADI | ASILIMIA | IDADI | ASILIMIA |
| Shule za mseto | 180 | 33.3 | 2 | 33.3 |
| Shule za wasichana | 180 | 33.3 | 2 | 33.3 |
| Shule za wavulana | 180 | 33.3 | 2 | 33.3 |
| **JUMLA** | **540** | **100** | **6** | **100** |

Jedwali 4.2 Linaonyesha kwamba asilimia 66.6 (4) ya walimu na asilimia 66.6 (360) ya wanafunzi walitoka katika shule za jinsia moja. Asilimia 333.3 (2) ya walimu na asilimia 33.3 (180) ya wanafunzi walitoka katika shule za mseto. Hii inaonyesha kuwa kulikuwa na wahojiwa wengi kutoka shule za jinsia moja ikilinganishwa na shule za mseto. Hata hivyo data hii inadhihirisha kuwa aina zote za shule; yaani shule za jinsia moja- za wavulana na za wasichana na shule za mseto zilishirikishwa katika utafiti na jambo hili liliboresha matokeo ya utafiti.


Kigezo cha jinsia ya walimu waliohojiwa kilizingatiwa ili kuimarisha ubora wa data. Jinsia ya walimu ilikuwa kama ifuatavyo katika mchoro wa 4.1.




**Mchoro 4. 1: Jinsia ya Walimu**

Ilibainika kuwa asilimia 30 ya walimu waliohojiwa ilikuwa ya kiume huku asilimia 70 ikiwa ya kike. Sifa hii ya kidemografia inadhihirisha kwamba kuna tofauti ya kijinsia inapohusu suala la ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari. Hali hii inakubaliana na maoni ya Babusa (2010), kuwa jinsia ya kike hufanya vyema sana katika masomo ya lugha na fasihi kuliko jinsia ya kiume.


Utafiti huu pia ulichunguza viwango vya elimu vya walimu wa fasihi kwa sababu kigezo hiki kinaweza kuathiri vigezo vikuu vinavyochunguzwa. Matokeo yake yalikuwa kama yanavyoonyeshwa katika mchoro 4.2




**Mchoro 4. 2: Kiwango cha Elimu cha Walimu wa Fasihi**

Matokeo haya yanaonyesha kuwa asilimia 75 ya walimu walihitimu shahada ya kwanza nayo asilimia 10 wana shahada ya uzamili huku asilimia 15 wakiwa na stashahada. Hili ni dhihirisho tosha kuwa wote walioshirikishwa katika utafiti huu walikuwa wamehitimu kufundisha fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, walimu hao wangeweza kuelewa vizuri masuala yanayohusiana na mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi zikiwemo changamoto za matumizi ya mbinu yenyewe. Richards na Wengine (2014), wanasema kuwa mafunzo ya kitaalamu na uhitimu wa walimu katika kazi yao ni mambo muhimu sana yanayowezesha walimu hao kuelewa vyema na kile wanachofundisha na kukifundisha ipasavyo.

Viwango vya tajriba ya walimu wa fasihi pia vilichunguzwa katika utafiti huu. Mchoro 4.3. unaonyesha matokeo ya kigezo hicho.





**Mchoro 4. 3:Tajiriba ya Ufundishaji wa Fasihi kwa Walimu**

Mchoro 4.3 unaonyesha kuwa walimu 6 walikuwa wamefundisha fasihi kwa muda wa miaka 6 hadi 10, na walimu 3 walikuwa na uzoefu wa mwaka 1 hadi 5. Walimu 2 walikuwa wamefundisha fasihi kwa kipindi cha miaka 11 hadi 15 huku mwalimu mmoja pekee akiwa na tajiriba ya miaka zaidi ya 15. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wengi wa walimu waliohojiwa walikuwa wamefundisha fasihi kwa zaidi ya miaka sita. Huu ulikuwa muda wa kutosha kwa walimu hao kuelewa mbinu zote zinazotumiwa kufundisha fasihi ya Kiswahili. Tajriba hii iliwawezesha walimu hao kutoa data iliyotakiwa kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundidhaji wa riwaya. Kwa mujibu wa Richards na Wengine

(2014), tajiriba ya mwalimu katika ufundishaji inamwezesha kutumia mbinu zote nzuri katika ufundishaji ili kuweza kuboresha matokeo ya mtihani ya wanafunzi wake.

### 4.3 Mbinu zinazotumiwa na Walimu wa Fasihi kufundishia Riwaya

Haya ndiyo yalikuwa madhumuni ya kwanza ya utafiti. Matokeo yake yalitokana na hojaji na mahojiano na walimu na yamewasilishwa katika mchoro wa 4.4 kama inavyoonyeshwa.




**Mchoro 4. 4: Matumizi ya Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na Walimu katika Ufundishaji wa Riwaya**

Kulingana na matokeo haya ni wazi kuwa idadi kubwa ya walimu 9 walitumia mbinu ya mhadhara kufundisha riwaya huku walimu 8 wakitumia mbinu ya masaili. Mwalimu mmoja akiunga mkono matumizi yake ya mbinu hizi mbili alisema kuwa *"Kwa kutumia mbinu ya mhadhara na masaili, mimi huweza kusomesha riwaya kwa muda mfupi na hivyo basi kutimiza mahitaji ya shule ya kukamilisha silabasi mapema."*

Walimu 2 walitumia mbinu ya mijadala ya darasani. Baadhi yao walielezea kuwa mbinu hiyo haipendwi na wanafunzi kwa vile huchukua muda mrefu kwa hivyo haitumiki sana. Nao walimu 5 walieleza kuwa wao hutumia mbinu ya ufundishaji wa marika. Mmoja wa waliotumia mbinu hii alielezea kuwa, *"ufundishaji wa marika huniwezesha kuokoa muda kwa kuweza kuwateua baadhi ya wanafunzi kuwafundisha wenzao na hivyo kufundisha mambo mengi yaliyomo kwa wakati mfupi."*

Walimu 7 walieleza kuwa wao hutumia mbinu ya usomaji kimya. Wao waliwaagiza wanafunzi wasome riwaya kimyakimya kivyao na hatimaye walimu waliwaongoza wanafunzi katika kuandika hoja muhimu kupitia mtindo wa imla. Wengi wao walielezea umuhimu wa mbinu hiyo kama iliyowasaidia kufundisha mambo mengi yaliyomo kwa muda mfupi. Aidha walimu 3 walitumia uigizaji huku waliotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi wakiwa wawili.

Kwa mujibu wa matokeo haya ni kwamba mbinu zinazotumiwa na walimu kwa wingi ni masaili, mhadhara na usomaji wa kimya uliounganika na imla. Hizi ni mbinu ambazo humwegemea zaidi mwalimu. Mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi kama vile mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, uigizaji na mijadala ya darasani hazitumiki sana na walimu wa riwaya ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na maoni ya Richard na Rodgers (2014), kuwa mbinu nyingi zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wao ni zile zinazowaegemea walimu wenyewe. Wasomi hawa wanaelezea zaidi kuwa mbinu hizi hazitimizi mahitaji ya kielimu ya wanafunzi. Huenda jambo hili ndilo chanzo cha matokeo mabaya ya wanafunzi katika mtihani wa fasihi. Ili kutimiza mahitaji ya wanafunzi

ya ufundishaji wa fasihi, walimu wanapaswa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya kwa kiwango cha juu.

## 4.4 Kiwango ambacho Walimu wa Fasihi hutumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Haya ndiyo yaliyokuwa madhumuni ya pili ya utafiti huu. Kutokana na uchunzaji darasani, hojaji na mahojiano na walimu ilibainika kwamba walimu 11 walifundisha fasihi andishi vipindi vitatu kwa juma huku hivyo vingine vitatu wakivitumia kufundisha vipengele vya lugha na fasihi simulizi.

Data ifuatayo iliweza kukusanywa kuhusu kiwango chao cha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

**Jedwali 4. 3: Kiwango cha Matumizi ya Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Juma**

| Matumizi | Idadi |
|---|---|
| Waliotumia mara tatu kwa juma | 1 |
| Waliotumia mara mbili kwa juma | 2 |
| Waliotumia mara moja kwa juma | 3 |
| Wasioitumia kabisa | 6 |
| **JUMLA** | **12** |

Kutokana na matokeo katika jedwali hili ilitokea wazi kuwa mwalimu mmoja (1) ndiye aliyetumia mbinu husika mara tatu kwa juma nao walimu wawili (2) wakaitumia mara mbili kwa juma. Walimu watatu (3) waliitumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi mara moja kwa juma. Walimu sita (6) walikiri kutoitumia mbinu hiyo kabisa katika ufundishaji wao darasani. Aidha, walikuwa na sababu mbalimbali za kutoitumia mbinu husika.

Kutokana na data hii ni wazi kuwa walimu wengi hawaitumii mbinu husika na wale waliotumia waliitumia kwa kiwango cha chini mno. Huenda hali hii ilichangiwa na hali ya kuwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huhitaji muda mwingi katika ufundishaji na mbinu ambazo huchukua muda mrefu huepukwa mno na walimu (Richards na Farrell, 2005). Kutoitumia mbinu hii au kuitumia kwa kiwango cha chini mno kunaashiria kuwa wanafunzi hawashirikishwi katika shughuli nzima ya ujifunzaji na ufundishaji. Kwa mujibu wa Richards and Renandya (2014), kufundisha wanafunzi bila kuwashirikisha katika kipindi kikamilifu huchangia kutoelewa kwao. Huenda tabia hii ya walimu imechangia matokeo mabaya katika somo la fasihi katika mtihani wa KCSE.

## 4.5 Athari za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Utendaji wa Wanafunzi

Haya yakiwa madhumuni ya tatu ya utafiti huu, data kuhusiana nayo zilikusanywa kupitia mtihani wa mwanzoni na mtihani wa mwishoni mwa utafiti. Shule mbili zilikuwa zimechaguliwa kwa kukusanya data ya aina hii huku kila shule ikiwa na makundi mawili ya wanafunzi yaani madarasa mawili.

Makundi yote manne ya wanafunzi yalipatiwa mtihani wa mwanzoni mwa utafiti. Matokeo ya mtihani huu tangulizi yalifanyiwa uchunguzi wa ‘t-test’ na kipimo chake cha “P- Value” kuwa juu ya 0.05. Hali hii iliashiria kuwa makundi hayo ya wanafunzi yalikuwa ya viwango sawa vya uelewa, jambo ambalo liliyafanya makundi hayo kuwa faafu kwa utafiti wa aina hii.

Baadaye, kundi moja la wanafunzi lilifundishwa vipengee vilivyohusu mbinu za uandishi wa riwaya kwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huku kundi la pili likifundishwa vipengele vivyo hivyo kwa kutumia mbinu za kawaida na

zilizozoeleka na walimu sana kama mhadhara, masaili na nyinginezo. Hatimaye makundi yote mawili yalipatiwa mtihani wa mwishoni mwa utafiti.

Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa mwishoni mwa utafiti ya makundi yote manne ya wanafunzi.

**Jedwali 4. 4: Matokeo ya Mtihani wa Mwishoni mwa Utafiti**

| **Kikundi** | **Idadi** | **Viwango vya usawa** | **Asilimia%** |
|---|---|---|---|
| Kundi la majaribio (I) $A_1$ | 43 | 30.52 | 76.3 |
| Lisilo la majaribio (I) $D_1$ | 44 | 16.90 | 42.3 |
| Kundi la majaribio (II) $A_2$ | 44 | 29.00 | 72.5 |
| Lisilo la majaribio (II) $D_2$ | 42 | 14.80 | 37 |


Matokeo ya mtihani katika makundi yote manne yalionyesha kuwa, wanafunzi katika makundi ya majaribio ($A_1$ na $A_2$) walifanya vyema wakilinganishwa na wenzao katika makundi yasiyokuwa ya majaribio ($D_1$ na $D_2$). Hali hii ilitokana na wanafunzi katika makundi ya majaribio kufundishwa kwa mbinu inayotegemea shughuli za wanafunzi. Wanafunzi katika makundi yasiyokuwa ya majaribio walifundishwa kwa mbinu za kawaida na zilizozoeleka mno miongoni mwa walimu. Matokeo yao ya mtihani yalionekana kuwa ya kiwango cha chini mno.

Kulingana na walimu waliosahihisha mtihani wa makundi yote manne, ilidhihirika wazi kuwa wanafunzi wa makundi ya majaribio walitoa majibu mengi yaliyoelezwa kwa kina. Majibu yenyewe hayakuwa na usawa wa mpangilio wa maneno. Nao wanafunzi wa makundi yasiyokuwa ya majaribio walitoa majibu yenye hoja chache na sawa kulingana na mpangilio wa maneno. Jambo hili linaaminika kusababishwa

na hali ya wanafunzi kutegemea mno hoja wanazopewa na mwalimu darasani wakati wa kufundishwa katika kujibu maswali kama anavyodai Kain (2003). Kwa mujibu wa Richard na Rodgers (2014), madarasa ya wanafunzi yanayofundishwa kwa kutumia mbinu intayotegemea shughuli za wanafunzi huwa na ushindani mkubwa. Katika madarasa ya aina hiyo kila mwanafunzi hujitahidi kwa uwezo wake ili kuweza kumshinda mwenzake. Jambo hili hudhihirika wakati wa mtihani pale wanafunzi wanapotoa majibu yenye hoja nzito na nyingi kuliko zile ambazo walipewa na walimu wao wakati wa kufundishwa darasani. Jambo ambalo lilidhihirika katika utafiti huu. Litakuwa jambo nzuri kwa walimu kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya ili kuimarisha uelewa wa wanafunzi.

### 4.5.1 Utendaji kwa Kutegemea Jinsia

Mtafiti pia alitaka kujua vile wanafunzi wanavyotenda kijinsia katika mtihani. Ili kubaini utendaji wa wanafunzi, kigezo cha jinsia ya wanafunzi waliofanya mtihani wa mwanzoni na mwishoni mwa utafiti kilizingatiwa. Jinsia ya watafitititiwa (wanafunzi) waliofanya mitihani ilikuwa kama inavyoonyeshwa katika mchoro 4.5




**Mchoro 4. 5: Jinsia ya Wanafunzi walioshiriki katika Mtihani.**

Matokeo haya yanadhihirisha kuwa asilimia 55 ya wanafunzi walioshirikikishwa katika mtihani wa utafiti walikuwa wasichana na wavulana wakiwa asilimia 45. Matokeo haya yalidhihirisha kwamba idadi kubwa ya wanafunzi walikuwa wasichana.

Katika kuchunguza utendaji wa wanafunzi kijinsia, mtafiti aliweza kugawa mitihani yote miwili, mtihani wa mwanzoni mwa utafiti na mtihani wa mwishoni mwa utafiti kijinsia, yaani katika makundi mawili. Matokeo ya mtihani ya wasichana yalilinganishwa na matokeo ya mtihani ya wavulana. Matokeo hayo yaliwasilishwa katika jedwali 4.5

**Jedwali 4. 5: Utendaji kwa kutegemea Jinsia**

| Kikundi | Idadi | Viwango vya usawa |
|---|---|---|
| Wasichana, mtihani 1 (Y1) | 95 | 24.60 |
| Wavulana, Mtihani 1 (Z1) | 78 | 16.0 |
| Wasichana, Mtihani 2 (Y2) | 95 | 27.0 |
| Wavulana, Mtihani 2 (Z2) | 78 | 17.8 |

Matokeo haya ya mtihani kuhusu utendaji wa wavulana na wasichana yanaonyesha kuwa makundi yote ya wasichana yalifanya vyema katika mtihani wa fasihi hasa riwaya. Kundi la kwanza (Y1) lilipata alama za usawa 24.6 nalo kundi la pili katika mtihani wa pili (Y2) likapata alama za usawa 27.0. Wavulana walionekana kupata alama za chini kuliko wasichana katika mitihani yote miwili. Katika mtihani wa kwanza, (Z1) wavulana walipata alama za usawa 16 na katika mtihani wa pili (Z2) wakapata alama za usawa 17.8. Matokeo hayo yalionyesha kuwa kwa jumla wasichana walifanya vyema katika mtihani wa fasihi hasa riwaya wakilinganishwa na wavulana. Matokeo haya yanaunga mkono utafiti wa Babusa (2010) aliposema katika utafiti huo wake kuwa jinsia ya kike hufanya vyema katika fasihi kuliko jinsia ya kiume.


## 4.6 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Madhumuni ya nne ya utafiti huu yalikuwa kubainisha mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Kutokana na hojaji na mahojiano na walimu, data zifuatazo ziliweza kukusanywa kuhusu suala hili. Jedwali 1.8 linaonyesha data kuhusu madhumuni haya.

**Jedwali 4. 6:Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi**

| Mtazamo | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Huipenda sana | 1 | 8 |
| Huipenda | 2 | 17 |
| Hawaipendi | 3 | 25 |
| Hawaipendi kabisa | 6 | 50 |
| **Jumla** | **12** | **100** |

Matokeo haya yameelezwa zaidi katika mchoro 4.6




**Mchoro 4. 6: Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi**

Kulingana na matokeo haya ni bayana kuwa mwalimu mmoja (1) ndiye aliipenda mbinu hii sana katika ufundishaji wake huku walimu wawili (2) wakiipenda kiasi, walimu watatu (3) hawakuipenda na walimu sita (6) hawaipendi kabisa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wao darasani. Matokeo

haya yanakubaliana na maoni ya Kang'ahi (2012), kuwa walimu wengi wana mtazamo hasi kuhusiana na mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kwa kuamini kwamba mbinu yenyewe huchukua muda mrefu wakati mwalimu anapoitumia katika kufundisha wanafunzi wake darasani. Miongoni mwa walimu 3 wanaoipenda mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi wawili walielezea kuwa mbinu hiyo ni mwafaka kabisa katika ufundishaji wa riwaya kwa sababu huwawezesha wanafunzi kuingiliana kwa muda mrefu wakitekeleza shughuli husika. Maoni yao yanaunga mkono utafiti wa Rost (2013).

Walimu sita (6) walieleza kuwa hawaipendi mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, walielezea zaidi kuwa msukumo wa kukamilisha silabasi mapema kutoka katika usimamizi wa shule hauwezi kuwaruhusu kuitumia mbinu hiyo hata kidogo katika ufundishaji wao wa riwaya.

### 4.7 Changamoto wanazokabiliana nazo Walimu wanapotumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Haya ndiyo yaliyokuwa madhumuni ya mwisho ya utafiti huu. Data kuhusiana na madhumuni haya zilikusanywa kupitia kwa hojaji, mahojiano na uchunzaji darasani. Jedwali la 4.7 linaonyesha data kuhusiana na swala hili.

**Jedwali 4. 7: Changamoto za Walimu katika Matumizi ya Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi.**

| Changamoto | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Muda mrefu unaotumiwa na wanafunzi wakitumia mbinu hii | 6 | 50 |
| Woga miongoni mwa wanafunzi wakati wa kuwasilisha darasani | 3 | 25 |
| Kazi nyingi kwa mwalimu akielekeza wanafunzi wakitumia mbinu husika | 5 | 42 |
| Wanafunzi wavivu kutoshiriki katika mijadala na uwasilishaji | 2 | 17 |
| Wanafunzi wajuaji kutowaruhusu wenzao kushiriki uwasilishaji | 1 | 8 |
| Wanafunzi werevu kuhisi kuwa wenzao wanawaharibia wakati | 2 | 17 |
| Baadhi ya Makundi kutotaka kuwasilisha kazi yao darasani | 3 | 25 |
| Baadhi ya wanafunzi kutokubaliana na mawasilisho ya wenzao | 2 | 17 |
| Ukesofu wa utulivu na amani ya kutosha katika makundi na wakati wa uwasilishaji | 3 | 25 |
| Mashindano miongoni mwa wanafunzi na mapingano yanayovuruga uwasilishaji | 2 | 17 |

Kulingana na matokeo haya, ilikuwa wazi kuwa changamoto kubwa miongoni mwa walimu katika kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, ilikuwa muda. Walimu sita (6) walitaja muda kuwa kikwazo kikubwa cha matumizi ya mbinu inayotetegemea shughuli za mwanafunzi darasani. Walieleza kuwa wanafunzi huhitaji muda mwingi wa kutekeleza shughuli na kuwasilisha mada zao mbele ya darasa na ambao haupatikani wakati wa kipindi.

Walimu watatu (3) walitatizwa na woga miongoni mwa baadhi ya wanafunzi. Woga wenyewe uliwafanya wanafunzi kadha wasishiriki katika shughuli hata kutowasilisha matokeo ya mijadala yao ya kazi ya makundi darasani mbele ya hadhira. Kulingana na Stewart na Shamdasani (2014), woga ni kikwazo kikubwa wakati wa kuwashirikisha wanafunzi darasani. Idadi kubwa ya walimu, walimu watano (5) walikuwa na changamoto ya kazi nyingi ya kuwaelekeza wanafunzi darasani wakitumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti wa Richard na Rodgers (2014) kuwa mbinu hii humhusisha mwalimu sana kuwakosoa wanafunzi katika makundi na wakati wa uwasilishaji. Jambo ambalo linaweza kuwa changamoto kubwa ikizingatiwa vipindi vingi walivyonavyo walimu wa fasihi vya kufundisha. Walimu wawili (2) walikuwa na changamoto ya wanafunzi wavivu kutoshiriki wakati wa mijadala ya vikundi na wakati wa uwasilishaji wa matokeo ya mijadala ya vikundi. Matokeo haya yaliunga mkono utafiti wa Kulik na Wenzake (2016). Walieleza kuwa baadhi ya wanafunzi hasa wale wavivu hawapendi kushirikishwa katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Mwalimu mmoja (1) alitaja changamoto ya wanafunzi werevu kutowaruhusu wenzao kuchangia. Jambo hilo kulingana na mwalimu husika huwavunja moyo wanafunzi wenye uwezo wa chini wa kiakili.

Aidha walimu wawili (2) walikuwa na changamoto ya wanafunzi werevu kuhisi kuwa wenzao wanawaharibia muda wao wakishirikiana nao katika shughuli husika. Walimu watatu (3) walihisi kuwa ni changamoto wakati baadhi ya makundi hawataki kuwasilisha kazi yao mbele ya wanafunzi wenzao baada ya kushiriki katika shughuli husika. Hali hii ilitokana na baadhi ya wanafunzi kuogopa kuulizwa

maswali kutokana na mawasilisho yao mbele ya darasa kulingana na mwalimu mmoja.

Kuna pia changamoto ya baadhi ya wanafunzi kutokubaliana na mawasilisho ya wenzio. Changamoto hii ilitajwa na walimu 2 (17%). Kulingana na mwalimu mmoja, hali hii huletwa na wanafunzi wenye uwezo wa kiakili wa juu wakilinganishwa na wenzao. Matokeo haya yanakubaliana na utafiti wa Suter na Busienei (2013) waliosema kuwa wanafunzi werevu mno wanaposhiriki katika mijadala darasani na wenzao wa kiwango cha chini cha uelewa, wao hudharau na kupuuza wenzao. Walimu watatu (3) walikuwa na changamoto ya ukosefu wa utulivu na amani wakati wa kutekeleza shughuli katika makundi na wakati baadhi ya wanafunzi wakiwasilisha matokeo ya mijadala yao ya makundi mbele ya darasa. Mwisho, walimu wawili (2) waliripoti mashindano na mapingano miongoni mwa wanafunzi wakati wa kutekeleza shughuli katika makundi na wakati wa uwasilishaji kama kikwazo kwa matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Ili kuimarisha ufundishaji wa riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kuna haja kubwa ya kukabiliana na changamoto hizi. Njia mojawapo ni kuwaandaa walimu vyema kabla ya matumizi ya mbinu hii katika ufundishaji.

# SURA TA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari na hitimisho ya utafiti huu. Aidha inatoa mapendekezo ya utafiti unaoweza kufanywa siku za usoni. Mapendekezo yanayotolewa yanajengeka kwenye msingi wa matokeo ya utafiti huu pamoja na malengo ya utafiti wenyewe.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Sehemu hii inashughulikia muhtasari na hitimisho ya matokeo kulingana na madhumuni ya utafiti wenyewe. Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa fasihi kufundisha riwaya. Aidha, ulikuwa na madhumuni ya kuchunguza kiwango ambacho walimu wa fasihi wanatumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Zaidi ya hayo utafiti ulichunguza athari za mbinu hiyo kwa utendaji wa wanafunzi. Kadhalika, utafiti ulibainisha mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Vilevile ulidhamiria kutambua changamoto ambazo walimu hukabiliana nazo wanapotumia mbinu hiyo.

### 5.2.1 Mbinu zinazotumiwa na Walimu wa Fasihi kufundisha Riwaya

Haya yakiwa madhumuni ya kwanza ya utafiti, ilibainika wazi kwamba mbinu ambazo zilitumiwa sana na walimu wa riwaya ni zile zilizoegemea upande wa mwalimu. Mbinu hizi ni kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili. Kama vile mtaalamu Biggs (2011) anavyosema katika utafiti wake, mbinu hizi za ufundishaji zinazomwegemea zaidi mwalimu zinapotumiwa, wanafunzi husoma

kijuujuu tu na huwa hawana uelewa wa ndani wa kile kinachofundishwa. Matokeo ya kusoma kijuujuu ni kufeli katika mitihani na kutoelewa kile kilichofundishwa.

Mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi kama vile mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi zilitumika kwa nadra sana na walimu wa riwaya. Mbinu hizo zinapotumika vizuri katika ufundishaji, wanafunzi huelewa kile kinachofundishwa kwa undani sana. Aidha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi humwezesha mwanafunzi mwenyewe kuwa mkakamavu na mwenye uwezo wa kusimama mbele ya wenzake bila woga. Haya hutokana na hali ya mwanafunzi huyo kuelewa vyema na kile kilichofundishwa na hivyo basi kujiamini zaidi mbele ya wenzake wakati wa mawasilisho darasani.

### 5.2.2 Kiwango ambacho Walimu wa Fasihi hutumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Haya ndiyo yaliyokuwa madhumuni ya pili ya utafiti. Kulingana na data, ilitokea wazi kuwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ilitumiwa kwa viwango vya chini mno katika ufundishaji wa riwaya. Ni mwalimu mmoja tu (1) aliyekuwa anaitumia mbinu hiyo mara tatu kwa juma. Walimu wengi hawakuitumia kamwe mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wao. Wengi wa walimu ambao hawakutumia mbinu husika katika ufundishaji wao walitoa sababu kuu kama muda mwingi unaohitajika katika kutumia mbinu hiyo na kazi nyingi ya mwalimu anaposhughulika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki katika shughuli husika.

Ili kuepuka kazi hiyo nyingi wengi wa walimu walionekana wakiepuka matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Ilibainika wazi kuwa iwapo walimu

hao wangetumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kwa kiwango cha juu bila shaka wangeimarisha uelewa wa wanafunzi wao wa somo la riwaya. Walimu walitakiwa kutumia mbinu hiyo kwa kiwango cha juu pamoja na kujitayarisha vilivyo kukabiliana na changamoto za matumizi ya mbinu hiyo darasani ili kuimarisha uelewa wa wanafunzi wao wa somo la riwaya.

#### 5.2.3.1 Athari za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa Utendaji wa Wanafunzi

Kuhusiana na madhumuni ya tatu ya utafiti, ilibainika wazi kuwa wanafunzi wanapofundishwa kwa mbinu hii, uelewa wao wa somo huwa wa kiwango cha juu wakilinganishwa na wanafunzi ambao wamefundishwa kwa kuzitumia mbinu za kawaida kama vile mbinu ya mhadhara na mbinu ya masaili. Kulingana na utafiti huu, wanafunzi wanapofundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huwa na uelewa wa ndani wa maswala yanayofundishwa. Katika kujibu maswali ya mitihani wanafunzi hao walitoa hoja nyingi kuliko wenzao waliokuwa wamefundishwa kwa mbinu za kawaida tu ambao hoja zao zilijikita tu madaftarini jinsi walivyokuwa wameandikiwa na walimu.

Wanafunzi waliofundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi walionekana kuwa na ubunifu tena wa kiwango cha juu wakilinganishwa na wenzao waliokuwa wamefundishwa kwa mbinu za kawaida. Kwa ujumla, ilibainika wazi kuwa wanafunzi waliofundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi walifanya vyema katika mtihani wakilinganishwa na wenzao ambao walifundishwa kwa mbinu za kawaida. Ni vyema wakati wote walimu kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli mbalimbali wakati wa kufundisha somo la riwaya ili wanafunzi waelewe vyema.

#### 5.2.3.2 Utendaji wa Wanafunzi kwa kutegemea Jinsia

Kuhusiana na suala hili la utendaji kwa kutegemea kigezo cha jinsia, mtafiti alibaini wazi kuwa wanafunzi wa jinsia zote mbili waliposhiriki katika mitihani miwili kulikuwa na tofauti za matokeo kutegemea kigezo cha jinsia. Wanafunzi wa jinsia ya kike walionyesha matokeo mazuri katika mtihani huku alama zao za usawa zikiwa juu ya alama ambazo wanafunzi wenzao wa jinsia ya kiume walipata katika mitihani ambayo ilikuwa sawa kwa jinsia zote mbili. Matokeo haya yaliashiria hali ambapo wanafunzi wa jinsia ya kiume walionyesha kulemewa na mtihani wa riwaya na kupata matokeo ya chini mno. Kutokana na matokeo haya ni wazi kuwa utendaji wa wanafunzi wa jinsia ya kiume katika masomo ya fasihi si wa kuridhisha. Huenda hali hii ilisababishwa na tabia ya wanafunzi wa jinsia ya kiume kuwa na mtazamo hasi kuhusu fasihi na kutoshiriki kikamilifu darasani wakati wa shughuli za ujifunzaji na ufundishaji. Kuna haja ya suala hili kuangaziwa katika kiwango cha juu na hatua kuchukuliwa ili wanafunzi wa jinsia ya kiume waweze kufanya vizuri katika mtihani wa fasihi.

### 5.2.4 Mitazamo ya Walimu kuhusu Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Haya yalikuwa madhumuni ya nne ya utafiti huu. Data zilizokusanywa ziliweza kutambua mitazamo ya walimu kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Ilibainika kuwa asilimia kubwa ya walimu hawaipendi mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, mbinu hii ikiwa miongoni mwa mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi. Walimu wengi waliohojiwa waliichukia sana mbinu hii kwa sababu licha ya kumshirikisha sana mwanafunzi katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji, inampatia mwalimu kazi nyingi ya kufuatilia

kipindi kwa makini hasa wakati wanafunzi wanapofanya shughuli zao wakiwa katika makundi. Aidha, kulikuwa na sababu zingine walizozitoa zilizowafanya kutopenda mbinu hii kama vile muda mwingi unaohitajika wakati wa matumizi yake miongoni mwa zingine.

Walimu wachache sana ndio walioeleza kuwa wanaipenda na kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Hao walieleza kuwa mbinu hii inapotumiwa vizuri huimarisha uelewa wa wanafunzi wa kina wa kile kinachofundishwa. Walimu wengi wanatakiwa kubadilisha msimamo wao hasi kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumiwa katika ufundishaji wa riwaya. Aidha walimu wawe na mtazamo chanya kuhusu mbinu hii na kuitumia kwa kiwango cha juu ili waweze kuimarisha ufundishaji wa riwaya.

### 5.2.5 Changamoto wanazokabiliana nazo Walimu wanapotumia Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi

Haya yakiwa madhumuni ya mwisho ya utafiti huu, walimu walipatikana kuwa na changamoto kadha katika matumizi ya mbinu hii. Changamoto hizo zilihusisha ukosefu wa muda wa kutosha wa kutekeleza mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi darasani. Pia, kazi nyingi iliyohusishwa na mbinu hii kwa upande wa walimu wakati wa kuelekeza wanafunzi wakitekeleza shughuli husika katika makundi. Aidha wengi wa wanafunzi hawakuipenda mbinu husika kwa kuwa iliwashirikisha sana katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Jambo hili liliwatatiza sana walimu walipokuwa wakitumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya.

Walimu wachache waliweza kukabiliana na changamoto zenyewe na wakatumia mbinu hiyo kufundishia huku wengi wao wakiamua kutumia mbinu zinazomwegemea mwalimu. Kwa kutumia mbinu za kawaida za kufundishia, walimu hukosa kufikia malengo yao ya ufundishaji wa riwaya. Walimu wote wanatakiwa kubuni mbinu za kukabiliana na changamoto za mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ili kuweza kufanikisha matumizi ya mbinu husika katika ufundishaji wa riwaya.

### 5.3 Hitimisho

Baada ya data kukusanywa kuhusiana na utafiti huu na kuchanganuliwa, ilibainika wazi kuwa walimu wa fasihi hasa riwaya hutumia mbinu za kawaida katika ufundishaji wao kama vile Mhadhara, Masaili, usomaji kimya na imla na kadhalika. Mbinu zinazowashirikisha wanafunzi kama vile mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi hazitumiki kwa wingi na walimu wa fasihi hasa riwaya.

Wanafunzi wanapofundishwa somo la riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huelewa vyema na kwa undani kile kinachofundishwa. Ufundishaji wa riwaya kwa kutumia mbinu zilizozoeleka na walimu na za kawaida huchangia katika matokeo mabaya ya wanafunzi katika mitihani ya fasihi. Wanafunzi husoma kijuujuu bila kuelewa kwa undani kile kinachofundishwa.

Licha ya walimu kadha kukubali kuwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi huchangia katika kuwezesha uelewa mzuri wa wanafunzi na kile kinachofundishwa, ni wachache mno walioitumia mbinu hiyo kwa kiwango cha juu darasani wakati wa ufundishaji. Mbinu hii iliepukwa na walimu pamoja na mbinu zingine zote zinazoegemea zaidi upande wa mwanafunzi. Kwa kufanya hivyo

walimu hao walichangangia uelewa mbaya wa somo la riwaya miongoni mwa wanafunzi kwa matumizi ya mbinu ambazo hazishirikishi wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Uelewa huo mbaya wa fasihi ulichangia katika matokeo mabaya ya somo la fasihi katika mtihani wa kidato cha nne (KCSE) miongoni mwa wanafunzi katika kaunti ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni.

Walimu wengi wa somo la riwaya walikuwa na changamoto kadha katika matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Changamoto ya ukosefu wa muda wa kutosha wa kutekeleza mbinu hii na kazi nyingi kwa mwalimu wakati wa kutumia mbinu yenyewe ndizo zilizokuwa kikwazo kikubwa kwa matumizi ya mbinu hiyo. Ni wazi kuwa changamoto hizi ni miongoni mwa changamoto nyingi zinazowakabili walimu katika matumizi ya mbinu zinazomwegemea zaidi mwanafunzi hasa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

Matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa somo la riwaya yanachangia uelewa mzuri wa riwaya miongoni mwa wanafunzi. Ili kuimarisha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya, walimu wanahitaji kuandaliwa vyema ili kukabiliana na changamoto zote na kuweza kutumia mbinu husika kwa kiwango cha juu katika ufundishaji wa riwaya. Aidha, walimu wanahitaji kubadilisha mtazamo wao kuhusu mbinu husika ili kuweza kuitumia bila ugumu wowote katika ufundishaji.

### 5.4 Mapendekezo

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuichanganua, alifanya mapendekezo yafuatayo ambayo yakizingatiwa na washikadau katika sekta ya elimu, inaaminika kuwa ufundishaji wa riwaya utaimarika: -

i) Ilipendekezwa kuwa walimu wa fasihi hasa riwaya watumie mbinu za ufundishaji zinazomwegemea zaidi mwanafunzi kama vile mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi, mijadala ya darasani, uigizaji na kadhalika. Katika mbinu hizo, mwalimu awe mwelekezi tu huku wanafunzi wakishirikishwa zaidi katika vipindi. Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ipewe kipaumbele katika ufundishaji wa somo la riwaya ili kuimarisha matokeo ya mtihani wa somo la fasihi wa wanafunzi wa kidato cha nne (KCSE).

ii) Walimu wa somo la riwaya katika shule za upili waache kabisa matumizi ya mbinu za kawaida katika ufundishaji kama vile mbinu ya mhadhara, imla na masaili kwa kuwa mbinu hizo zinachangia katika uelewa mbaya wa somo la fasihi miongoni mwa wanafunzi, hali inayosababisha matokeo mabaya ya wanafunzi katika mtihani wa fasihi wa kidato cha nne.

iii) Warsha za walimu ziweze kuandaliwa ili kuwaandaa walimu zaidi kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya. Katika warsha hizo walimu waelekezwe jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazozuka wakati wa matumizi ya mbinu husika ili waweze kukabiliana na vikwazo hivyo wakati wa ufundishaji wa somo la riwaya wakitumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi. Aidha, katika warsha hizo walimu waelekezwe ipasavyo kuhusu umuhimu wa mbinu hii katika ufundishaji wa somo la riwaya ili wabadili mtazamo wao hasi kuhusu mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi.

iv) Vyuo vikuu vya walimu visisitize matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi pamoja na mbinu zote zinazomshirikisha mwanafunzi vyema katika ufundishaji wa fasihi hasa riwaya wakati wa ufundishaji wa walimu. Aidha, walimu waandaliwe vya kutosha kuhusiana na matumizi yao ya mbinu zinazomwegemea mwanafunzi na hasa mno matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi ili waweze kubadili mtazamo wao hasi kuhusu matumizi ya mbinu hii katika ufundishaji wa riwaya na fasihi kwa jumla. Hali kadhalika, walimu wafundishwe kuhusu umuhimu wa kuwa na mtazamo chanya kuhusiana na mbinu wanazotumia katika ufundishaji. Aidha jinsi jambo hilo linavyoathiri matumizi ya mbinu husika pamoja na uelewa wa wanafunzi wao.

**5.5 Mada zinazopendekezwa kwa Utafiti zaidi**

Kwa kuwa utafiti huu ulihusu matumizi mbinu inayotegemea shughuli katika ufundishaji wa riwaya, tafiti zaidi zinapendekezwa katika mada zifuatazo: -

i) Utafiti ufanywe kuhusu mbinu za ufundishaji wa hadithi fupi, ushairi na tamthlia katika shule za upili.

ii) Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli katika ufundishaji wa fasihi katika shule za msingi.

iii) Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika maeneo mengine nchini kuhusiana na matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli katika ufundishaji wa fasihi na matokeo kulinganishwa na ya utafiti huu.

# MAREJELEO


Ahmad, F. na Aziz, J. (2009). Students' Perceptions of the teachers of Literature Communicating and Understanding Through the Eye of Audience. *European Journal of Social Science, 7(3) 17.*

Al, A. A. G. M. G. (2017). A Critical Review of The Importance of Medium Term Planning for Islamic Education. *Journal of Education and Social Sciences, (8) 4, 25-9.*

Amineh, R. J., & Asl, H. D. (2015). Review of Constructivism and Social Constructivism. *Journal of Social Sciences, Literature and Languages, 1(1), 9-16.*

Babusa, H. (2010). Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya. Unpublished Ph.D. Thesis Kenyatta University.

Bakize, L. H., Ngugi, P. M. Y., & Lyimo, E. B. (2018). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto nchini Tanzania na Kenya: Mkabala Linganishi. *Kiswahili, 80(1).*

Benton, M. & Fox, G. (1985*). Teaching Literature Nine to Fourteen.* New York: Oxford University Press.

Bhattacharjee, J. (2015). Constructivist approach to learning – an effective approach of Teaching learning. *International Research journal of Interdisciplinary & Multidisciplinary Studies, 1(4), 23-28.*

Biggs, J. B. (2011). *Teaching for quality learning at University: What the student does:* MC Graw – Hill Education (UK).

Calvert, M., & Sheen, Y. (2015). Task-based language learning and teaching: An action- research study. *Language Teaching Research, 19(2), 226-244.*

Carless, D. (2012). Task –based language teaching in confucian-heritage settings prospects and Challenges on task: *The Journal of the JALT Task-based learning S/G.*

Chang, Y. (2010). Students' perceptions of Teaching styles and Use of learning strategies. Retrieved from http.//trace.tennessee.edu/ukgradthes/782 on 27/8/2016.

Chetty, R., Friedman, J.N. & Rockoff, J.E (2014). Measuring the impact of teachers; Evaluating bias in teacher value-added estimates, The American value-added estimates. *The American Economic Review, 104(9), 2593-2632.*

Creswell, J. W. (2013). *Research design qualitative quantitative and mixed methods approaches.* Sage publications

Ellis, R. (2003). *Task-based language learning and teaching*. Oxford, UK: Oxford University Press.

Eldredge, J. L. & Butterfield, D. (1986). Alternatives to Traditional Reading Instruction – The Reading Teacher. *International Literacy Association. Vol. 40 (1) pp 32-37*

Ferguson, P. (2014). Co-operative Learning and Critical thinking. *Secondary Schools and Cooperative Learning: Theories, Models and Strategies, 55.*

Gathumbi, A. (1995). Verbal Discourse Events in a Bilingual Formal Setting: Instructional Procedures in Esl classrooms in Kenyan Secondary Schools. Unpublished M.Ed. Thesis, Kenyatta University.

Gathunga, J. K. (2012). Makosa ya Kisintaksia katika Uandishi wa Insha za Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Upili. M.A. Thesis. Kenyatta University.

Gituku, N. (1990). Maigizo ya Kienyeji ya Watoto nchini Kenya. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Gromov, M.D. (2009). Children's Literature in Kenya. A mirror of Kenyan Culture. *A Journal of language Technology and Entreprenuership in Africa Vol 1 (2). PP 198- 207.*

Henson, K. T. (2015). *Curriculum Planning: Integrating Multiculturalism, Constructivism And Educational reform.* Waveland Press.

Hill, A. (2018). Manufacturing the African Literary Canon. The Rise of the African Novel: Politics of Language, Identity, and Ownership, 133.

Hill, C. P. (2017). 14 Some Developments in Language and Education in Tanzania since 1969. *Routledge Revivals: Language in Tanzania (1980), 362.*

Jamhuri ya Kenya (2010). *Katiba Iliyoidhinishwa ya Kenya.* Nairobi: Government Printing Press.

John, P. (2018). Constructivism: Its implications for Language Teaching and Second Language Acquisition. *Paper in Education and Development (33-34)*

Kain, D.J. (2003). Teacher Centered Versus Student Centered: Balancing Constraint and Theory in the Composition Classroom. *Pedagogy, 3(1), 104 – 108*

Kang'ahi, M. (2012). Teaching styles and Learners' Achievement in Kiswahili Language in Secondary Schools. *International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development.*

Kemper, E.A., Stringfield, S., & Teddlie, C. (2003). Mixed Methods Sampling Strategies in Social Science Research. *Handbook of Mixed Methods in Social and behavioural Research, 273-296.*

Kenya, L. O. (2010). *The Constitution of Kenya, 2010.* Attorney General: Nairobi.

Kimani, J. N. (2015). Uhusiano wa Mbinu za Kufundishia Sarufi na Umilisi wa Mazungumzo ya Wanafunzi wa Sekondari, Kaunti ndogo ya Thika Magharibi, Kenya.Tasnifu ya M. Ed; Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kimberlin, C.L., & Winterstein, A. G. (2008). Validity and Reliability of Measurement Instruments Used in Research. *Am J Health Syst Pharm, 65(23), 2276-84*.

KNEC, (2017). *KCSE Report: 2012-2017*. Nairobi: Top Rank Publishers.

Kombo, D. & Tromp, D. (2006). *Project and Thesis Writing; An Introduction*. Nairobi: Pauline Publishers.

Kothari C.R. (2004). *Research Methodologies. Methods and Techniques*. New Delhni: New Age International Publisher.

Kulik, J.A., Kulik, C.& Carmichael, D. (2016). Keller Plan. Retrieved April 10. 2017.

Mangeni, E.N. (2010). Learners' Verbal Communication in English Language During Classroom Interaction in London Division, Kipkelion District. Unpublished Thesis, Kenyatta University.

Matei, A.K. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishing and Media Services limited.

Miima, F.A. (2014). Integration of Information Communication Technologies in Teaching and Learning of Kiswahili Language in Public Secondary Schools in Kakamega County, Kenya. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Momanyi, C. (2007). *Nafasi ya lugha ya Kiswahili katika Elimu ya Vyuo Nchini Kenya, In Kimani Njogu (Mh) Kiswahili na Elimu Nchini Kenya.* Nairobi: Twaweza Communications.

Moshi, L. (2006). The globalized world languages: The case of Kiswahili. In Selected proceedings of the 36th annual conference on African linguistics (pp. 166-175). Somerville: Cascadilla Proceedings Project.

Musau P.M. & Chacha, L.M. (2001). *Mbinu za kisasa za kufundishia Kiswahili*. Nairobi: KLB.

Mugenda O.M. & Mugenda, A.G. (2003*) Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts press.

Nardi, P. M. (2018). *Doing Survey Research: A guide to Quantitative Methods.* Routledge.

Ngugi, P.M. (2009). Language and Literacy Education. The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Wieu (Haijachapishwa).

Njogu, K.& Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nunan, D. (2006). *Task-based Language Teaching.* Ernst Klett Sprachen.

Odaga, A. (1985). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bereau.

Orodho, J.A. (2009*). Elements of Education and Social Science Research Methods*. Maseno: Kanezja publisher.

Orodho, J.A. (2003). T*echniques of Writing Research Proposal and Reports in Education and Social Sciences. (2nd ED).* Nairobi Kanezja HP. Enterprise.

Osazee, F.P. (2004). Not only Books for Africa but a reading culture Too. Keynote Address presented at the 29th IBBY Congress Cape Town. South Africa 5-9thSeptember 2004.

Pulido, F., Catalina, D., & González Mesa, P. A. (2016). Using task-based learning approach to foster oral production in 8° graders (Doctoral dissertation, Corporación Universitaria Minuto de Dios).

Richards, J.C. & Farrell, T.S.C. (2005). *Professional development for language teachers:strategies for teacher learning.* Ernst Kleff Sprachen.

Richard, J.C. & Rodgers, T.S. (2014). *Approaches and Methods in Language Teaching.*Cambridge University Press.

Richards J.C. & Renandya, W.A. (2014). *Methodology in Language Teaching: An Anthology of Current Practise.* Cambridge University Press.

Rost, M. (2013). *Teaching and Researching:* Listening. Routledge.

Rubio, D. M., Berg-Weger, M., Tebb, S. S., Lee, E. S., & Rauch, S. (2003). Objectifying content validity: Conducting a content validy study in social work research. *Social Work Research, 27(2), 94-104.*

Sadoski, M., & Paivio, A. (2013). *Imagery and Text: A Dual Coding Theory of Reading and writing.* Routledge.

Stewart, D.W. & Shamdasani P.N. (2014). *Focus groups: Theory and Practice (vol.20*). Sage Publications.

Suter, E. & Busienei, A.J. (2013). Materials and Instructional Approaches used by Secondary School Teachers of Kiswahili Oral Literature in Markwet District, Kenya. *Jounal of Emerging Trends in educational Research and policy studies(JETERAPS), 4(3), 566-572*

Twoli, N.W., Maundu. J. N., Muindi, D.M., Kiio, M. & Kithinji, C.T. (2007) *Instructional Methods in Education: A Course Book for General Teaching Methods*. Nairobi: KIE.

TATAKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Oxford: Nairobi University Press.

Ur, P. (2013). Language –Teaching Methods Revisited. *ELT Journal, 67(4), 468-474.*

Valsiner, J., & Rosa, A. (2007). Contemporary Socio-Cultural Research. *The Cambridge Handbook of Socio-Cultural Psychology, 1-20.*

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo Cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2003); *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Yu, G. (2008). Cooperative Learning for Heterogenous EFL Classroom in Secondary Schools in Taiwan. *Journal of Kaohsiung Normal University*.

Zheng, X. & Borg, S. (2014). Task-based learning and teaching in China: Secondary school teachers' beliefs and practices. *Language Teaching Research, 18(2), 205-221.*

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO CHA 1: HOJAJI KWA WALIMU

**Maagizo kwa walimu**

Utafiti huu unadhamiriwa kwa madhumuni ya kielimu tu. Utalenga kuchunguza namna mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inavyotumiwa katika kufundishia riwaya miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili katika kaunti-ndogo ya Mukaa, kaunti ya Makueni, nchini Kenya.

Hojaji hii imegawanyika katika sehemu kadha. Tafadhali jibu maswali yote kwa uaminifu. Mtafiti anakujuza kuwa habari utakayotoa itakuwa siri na itatumiwa kwa utafiti huu tu. Tia alama sahihi (√) panapofaa au ujaze habari inayohitajika katika nafasi zilizoachwa.

### Sehemu ya Kwanza: Habari/ Maelezo ya Kibinafsi

Sehemu hii inadhamiria kutafuta habari/maelezo kukuhusu wewe na pia kuhusu shule yako.

1. Jinsia ya mwalimu

   Mke ☐

   Mume ☐

2. Umri wa mwalimu

   Miaka 21-30 ☐

   Miaka 31-4 ☐

   Miaka 41-50 ☐

   Zaidi ya 50 ☐

3. Kiwango cha masomo cha mwalimu

- Uzamili ☐
- Shahada ya kwanza ☐
- Diploma ☐
- Stashahada ☐

4. Umefundisha kwa muda gani?

- Miaka 0-5 ☐
- Miaka 6-10 ☐
- Miaka 11-15 ☐
- Zaidi ya 15 ☐

5. Shule yako ni ya aina gani?

- Ya Kitaifa ☐
- Ya Kaunti ☐
- Ya Kaunti-ndogo ☐

6. Idadi ya wanafunzi

- Chini ya 200 ☐
- Kati ya 201-300 ☐
- Kati ya 301-400 ☐
- Zaidi ya mia 400 ☐

## Sehemu ya Pili: Mbinu Zinazotumiwa katika Ufundishaji

Sehemu hii inadhamiria kukusanya data kuhusu suala linalotafitiwa

1. Unafundisha vipindi vingapi kwa wiki?

   Chini ya kumi 10 ☐

   Kati ya 11-20 ☐

   Kati ya 21-30 ☐

   Zaidi ya 30 ☐

2. Ni vipindi vingapi vimetengewa somo la Kiswahili kwa wiki?

   Vinne ☐

   Vitano ☐

   Sita ☐

   Zaidi ya sita ☐

3. Kati ya hivyo vipindi vya Kiswahili, ni vingapi hutumiwa kufundishia fasihi andishi?

   Viwili ☐

   Vitatu ☐

   Vinne ☐

   Zaidi ya vinne ☐

4. Ni mbinu gani ya ufundishaji ambayo unatumia kufundishia riwaya mara nyingi?

Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi

Masaili ☐

Mhadhara ☐

Nyinginezo ☐

Ikiwa ni nyinyine, itaje…………………………………………………….

5. Je, wewe hutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia riwaya mara ngapi kwa juma?

Mara moja ☐

Mara mbili ☐

Mara tatu ☐

Zaidi ya mara tatu ☐

6. Wanafunzi hushirikishwa katika shughuli kwa muda gani wa kipindi?

Dakika 20 ☐

Dakika 15 ☐

Chini ya dakika 10 ☐

Dakika tano 5 ☐

**Sehemu ya Tatu: Athari za Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi kwa utendaji wa Wanafunzi**

1. Je, wewe huipenda mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi?

Huipenda sana ☐

Huipenda ☐

Siipendi ☐

Siipendi kabisa ☐

2. Kwa maoni yako, mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi hutimiza kwa kiwango kipi malengo ya kufundishia riwaya?

Hutimiza kabisa ☐

Kwa kiwango cha juu ☐

Kiwango cha kati ☐

Kiwango cha chini ☐

3. Ni kwa kiwango kipi ambacho wanafunzi wako huelewa somo la riwaya wanapofundishwa kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi?

Huelewa kabisa ☐

Kiwango cha juu ☐

Kiwango cha kati ☐

Hawaelewi ☐

**Sehemu ya Nne: Mitazamo ya Walimu na Changamoto za Matumizi ya Mbinu inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi.**

1. Ni mambo gani ambayo hutatiza matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji?

Mwelekeo wa wanafunzi ☐

Mwelekeo wa mwalimu ☐

Muda wa kusoma ☐

Mambo mengine ☐

Iwapo ni mengine
eleza_______________________________________________________

2. Je, ufundishaji wa riwaya kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi unafaa?

Ndio ☐

La ☐

Eleza _______________________________________________________________

3.Eleza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuimarisha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi

**Kiambatisho 2: Mwongozo wa Uchunzaji Darasani**

Shule ______________________________________Muda__________________

Darasa_______________________________ Tarehe________________________

| Shughuli | Matokeo |
|---|---|
| 1.Mbinu ya ufundishaji inayotumika | • Mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi<br>• Mhadhara<br>• Masaili au nyinginezo |
| 2. Kiwango cha matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi | • Cha juu<br>• Cha chini |
| 3.Mpangilio wa somo kwa kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi | • Upo<br>• Haupo |
| 4. Ujuzi wa mwalimu katika kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi | • Mzuri<br>• Wastani<br>• Usioridhisha |
| 5. Mwalimu anahusika katika kipindi kuwakosoa wanafunzi | • Ndio<br>• La |
| 6.Kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli husika | • Ndio<br>• La |
| 7.Muda uliopangiwa kipindi | • Unatosha<br>• Hautoshi |
| 8.Wanafunzi walifurahia kipindi | • Ndio<br>• La |
| 9. Malengo ya kipindi | • Yaliafikiwa<br>• Hayakuafikiwa |

**Kiambatisho cha 3: Mahojiano na Walimu wa Fasihi, Kidato cha Tatu**

1. Kwa nini unapenda kufundisha fasihi ya Kiswahili?

2. Ni mbinu gani unatumia sana unapofundisha riwaya?

3. Je, wewe hutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia riwaya?

4. Ni kwa nini wanafunzi wanapenda au hawaipendi mbinu hii?

5. Ni matatizo gani unayokabiliana nayo unapotumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi darasani?

6. Kulingana nawe, mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi inapotumiwa kufundishia riwaya, malengo ya somo huafikiwa?

7. Wewe kama mwalimu unafurahia kutumia mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi kufundishia riwaya? Eleza jibu lako.

**Kiambatisho Cha 4: Mtihani Tangulizi (Pre-Test)**

Maswali katika mtihani huu yatalenga kutathmini uelewa wa vipengele kadha vya riwaya kabla ya wanafunzi kufundishwa kwa mbinu tofauti kwa kila kikundi.

Mtihani huu ni wa wanafunzi wa kidato cha tatu. Maswali yanatolewa katika riwaya ya Chozi la Heri iliyoandikwa na Assumpta K. Matei. Alama zote ni arobaini.

## Swali la Kwanza

Eleza sifa za wahusika wafuatao katika riwaya ya Chozi la Heri

(a) Ridhaa

(b) Umulkheri (Alama 20)

**Swali la Pili**

Jadili maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika Riwaya ya Chozi la Heri

(Alama 20)

**Kiambatisho cha 5: Mtihani wa Mwishoni (Post – test)**

Maswali katika mtihani huu yatalenga kutathmini uelewa wa vipengele kadha vya riwaya baada ya baadhi ya wanafunzi kufundishwa kwa mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi na wengine kwa mbinu zingine.

Mtihani huu ni wa wanafunzi wa kidato cha tatu. Maswali yametolewa katika riwaya ya Chozi La Heri, iliyoandikwa na Assumpta K. Matei. Alama zote ni Arobaini

**Swali la kwanza**

Kwa kutoa mifano, jadili matumizi kumi ya kinaya katika riwaya ya Chozi la Heri.

(alama 20)

**Swali la pili**

Eleza jinsi mwandishi ametumia mbinu ya majazi katika riwaya ya Chozi la Heri na utoe mifano. (alama 20)

**Kiambatisho cha 6: Barua ya Ukubalifu wa Pendekezo la Utafiti (Chuo Kikuu cha Kenyatta)**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 020-8704150

Internal Memo

**FROM:** Dean, Graduate School

**DATE:** 4th September, 2018

**TO:** **Mr. Juliens Mumangi Koka**
**C/o Department of Educ. Communication & Technology**

**REF:** E55/CE/28028/2013

**SUBJECT:** **APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

==============================================

This is to inform you that Graduate School Board, at its meeting on **30th January, 2019**, approved your Research Proposal for the M.Ed. Degree entitled, **"Matumizi ya Mbinu Inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi Katika Ufundishaji wa Riwaya, Shule za Upili, Kaunti ya Makueni, Kenya."**

You may now proceed with your Data collection, subject to clearance with the Director General, National Commission for Science, Technology & Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking Forms per semester. The form has been developed to replace the Progress Report Forms. The Supervision Tracking Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

**JACKSON LUVUSI**
**FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL**

CC. Chairman, Department of Educational Communication & Technology

**Supervisors:**

1. Dr. Hamisi O. Babusa
   C/o Department of Educ. Communication & Technology
   **Kenyatta University**

2. Dr. Florence A. Miima
   C/o Department of Educ. Communication & Technology
   **Kenyatta University**

**Kiambatisho cha 7: Barua ya Idhini ya Utafiti (Chuo Kikuu Cha Kenyatta)**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 020-8704150

**Our Ref: E55/CE/28028/2013**

**DATE:** 4th February, 2019

Director General,
National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MR. JULIENS MUMANGI KOKA – REG. NO. E55/CE/28028/13**

I write to introduce Mr. Juliens Mumangi Koka who is a Postgraduate Student of this University. He is registered for M.Ed. degree programme in the **Department of Educational Communication & Technology.**

Mr. Koka intends to conduct research for a M.Ed. thesis Proposal entitled, **"Matumizi ya Mbinu Inayotegemea Shughuli za Mwanafunzi Katika Ufundishaji wa Riwaya, Shule za Upili, Kaunti ya Makueni, Kenya."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

**PROF. ELISHIBA KIMANI**
**DEAN, GRADUATE SCHOOL**

JL/cww


**Kiambatisho cha 8: Kibali cha Utafiti (NACOSTI)**

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. JULIENS MUMANGI KOKA***
**of KENYATTA UNIVERSITY, 181-90132**
**SULTAN HAMUD, has been permitted to**
**conduct research in *Makueni County***

**on the topic: *MATUMIZI YA MBINU INAYOTEGEMEA SHUGHULI ZA MWANAFUNZI KATIKA UFUNDISHAJI WA RIWAYA, SHULE ZA UPILI, KAUNTI YA MAKUENI, KENYA***

**for the period ending:**
***23rd April,2020***

**Permit No : NACOSTI/P/19/56996/29537**
**Date Of Issue : 23rd April,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



..............................
***Applicant's Signature***

..............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013**

**The Grant of Research Licenses is guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014.**

**CONDITIONS**

1. **The License is valid for the proposed research, location and specified period.**
2. **The License and any rights thereunder are non-transferable.**
3. **The Licensee shall inform the County Governor before commencement of the research.**
4. **Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.**
5. **The License does not give authority to transfer research materials.**
6. **NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project.**
7. **The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report within one year of completion of the research.**
8. **NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.**

**National Commission for Science, Technology and innovation**
**P.O. Box 30623 - 00100, Nairobi, Kenya**
**TEL: 020 400 7000, 0713 788787, 0735 404245**
**Email: dg@nacosti.go.ke, registry@nacosti.go.ke**
**Website: www.nacosti.go.ke**

**REPUBLIC OF KENYA**

**NACOSTI**

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEARCH LICENSE**

**Serial No.A 24162**

**CONDITIONS: see back page**

**Kiambatisho cha 9: Barua ya Idhini (NACOSTI)**

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471, 2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/19/56996/29537**

Date: **23rd April, 2019**

Juliens Mumangi Koka
Kenyatta University
P. O. Box 43844-00100
**NAIROBI.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya, shule za upili, Kaunti ya Makueni, Kenya"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Makueni County** for the period ending **23rd April, 2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Makueni County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**DR. STEPHEN K. KIBIRU, PhD.**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Makueni County.

The County Director of Education
Makueni County.

*National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001:2008 Certified*

**Kiambatisho cha 10: Barua ya Idhini (Mkuu wa Kaunti, Makueni)**

HARAMBEE

**THE PRESIDENCY**
**MINISTRY OF INTERIOR AND COORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT**

**Telegram:**
**Telephone: 0743-987-177**
**Fax:**
**Email: cc.makueni@interior.go.ke**

**COUNTY COMMISSIONER**
**MAKUENI COUNTY**
**P.O. Box 1-90300**
**MAKUENI**

8th May, 2019

**Ref**: MKN/CC/ADM.6/1 VOL.III/203

Juliens Mumangi Koka
Kenyatta University
P.O. Box 43844 – 10100
**NAIROBI**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Reference is made to Director General National Commission for Science Technology and Innovation letter **Ref. NACOSTI/P/19/56996/29537** dated **23rd April, 2019** on the above subject.

You are hereby authorized to undertake research on ***"matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya, shule za upili, Kaunti ya Makueni, Kenya "*** for a period ending **23rd April, 2020.**

By a copy of this letter the Deputy County Commissioner, Mukaa Sub County is requested to give you the necessary assistance.

B, K, NICHOLAS
FOR: COUNTY COMMISSIONER
**MAKUENI**

c.c.
County Director of Education
**MAKUENI**

Deputy County Commissioner
**MUKAA**

**Kiambatisho cha 11: Barua ya Idhini (Mkurugenzi wa Elimu, Makueni)**

REPUBLIC OF KENYA

**MINISTRY OF EDUCATION**

**STATE DEPARTMENT OF BASIC EDUCATION**

**Telephone: ..............**
**Fax: ......................**
*Email:cdemakueni@gmail.com*
***When replying please quote***

**Ref No. MKN/C/ED/5/33/VOL.2/175**

*COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION*
*MAKUENI COUNTY*
*P.O. BOX 41 - 90300*
*MAKUENI*

**8th May ,2019**

Sub-county Director of Education
**Mukaa Sub - County**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR JULIENS MUMANGI KOKA**

The office is in receipt of letter from the Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) authorizing Mr. Juliens Mumangi Koka of Kenyatta University to carry out research on **"Matumizi ya mbinu inayotegemea shughuli za mwanafunzi katika ufundishaji wa riwaya, shule za upili, Kaunti ya Makueni, Kenya"** for the period ending 23rd April, 2020.

Kindly accord him the necessary assistance.

COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
DATE: 8/5/2019
P.O. BOX 41-90300
MAKUENI
MAKUENI COUNTY - MOEST

Jesse K. Mwangi
For: County Director of Education
**Makueni County.**

**Kiambatisho cha 12: Ramani ya Kaunti -Ndogo ya Mukaa**

